BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT
1,008,534,842/-
KWA 1000/- TU!
SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 4

**SPIKA** aweka sawa kauli zinazopishana za waziri na mbunge


BUFE
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Kwanini kuna Sensa ya Majengo kwa mara ya kwanza nchini mwaka huu ?
Siri ya Wamasai kuwa walinzi mahiri na wauza dawa mijini

UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII


Ijumaa Juni 24, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580986

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


# Kauli ya CCM Katiba Mpya yashtua



UKURASA 2



FREEMAN MBOWE
**AMEDUMU NA HOJA WAKATI WOTE**



JAJI WARIOBA
**ALIONGOZA MCHAKATO**



DUNI HAJI - ACT
**ABARIKI HOJA, ADAI HATUA ZAIDI**



Katibu wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Kenani Kihongosi (katikati), akiongoza vijana kwenye matembezi yaliyoanzia Uwanja wa Benjamini Mkapa hadi viwanja vya Mwembe Yanga Temeke, mkoani Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa uhamasishaji wa Sensa ya Watu na Makazi, inayotarajiwa kufanyika Agosti 23 mwaka huu. **PICHA: SABATO KASIKA**

UKURASA WA 2

## MBARONI AKITUHUMIWA KUUA MWANAMKE 'GESTI'

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linamshikilia Heri Chisanga (33), mkazi wa Mburahati, kwa tuhuma za kumuua...

UKURASA WA 5

## TAASISI YA RUGE MUTAHABA KUZINDULIWA RASMI JUMAPILI



TAASISI ya Ruge Mutahaba inatarajiwa kuzinduliwa rasmi keshokutwa mkoani Dar...

UKURASA WA 5

## JIJI LATOA UFAFANUZI WAUZAJI MAGAZETI

JIJI la Dar es Salaam limetoa ufafanuzi kuhusu kilichoripotiwa dhidi ya wauzaji wa magazeti...

# Mabeyo ataja mitihani jeshini

**KIMO** kifo cha Rais Magufuli...*Endelea Ukurasa 2*

## Wakili wa kina Mdee atoa kauli kifuatacho

UKURASA 19

**MICHEZO** JEURI YAENDELEA KUTAWALA YANGA UK.24 | MAONI, KATUNI UK.6




Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (watatu kushoto), Mwenyekiti wa Kampuni ya Superdoll, Seif Ali Seif (wapili kushoto), aliyekuwa Mkurugenzi wa Biashara wa Michelin, Fred Stoeffler (kushoto), Rais wa Michelin Afrika, India na Mashariki ya Kati, Gaganjot Singh (watatu kulia) na Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Nabil Hajlaoui (wapili kulia), kwa pamoja wakikata keki katika maadhimisho ya miaka 30 ya Ushirikiano wa Superdoll na kampuni ya Michelin, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Kauli ya CCM Katiba Mpya yashtua upinzani

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kusisitiza umuhimu wa kuwapo kwa Katiba Mpya, Chama cha ACT-Wazalendo kimepongeza huku CHADEMA wakiamua kuitisha kikao cha Kamati Kuu kujadili suala hilo kabla ya kutoa tamko.

Juzi, Katibu wa Halmashauri Kuu wa CCM Taifa (NEC) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alitangaza CCM kinasisitiza umuhimu huo kwa kuzingatia mazingira ya sasa na kuangalia namna bora ya kufufua na kukwamua mchakato wake.

Akizungumza na Nipashe kuhusu kauli hiyo iliyotokana na vikao vya juu vya chama hicho kikiwamo cha NEC kilichofanyika Dodoma, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema wamewasikia wanzao wa CCM na wamepanga kuitisha kikao cha Kamati Kuu.

"Tumewasikia wenzetu wa CCM kuhusu Katiba Mpya, kwa sasa tutaitisha kikao cha Kamati Kuu na itajadili na hatimaye kutoa tamko lake siku za usoni.

Hivyo, tutawajulisha baada ya kikao husika kukaa," alisema.

Wakati CHADEMA wakijipanga kwa hilo, ACT-Wazalendo walitoa taarifa jana kupitia Katibu wa Habari, Uenezi, Mawasiliano na Umma Taifa, Salim Bimani, kikipongeza kauli hiyo ya CCM.

"Hatua hii ni kubwa, Mwenyekiti wa Taifa wa chama chetu, Juma Duni Haji, amefarijika kuwa mazungumzo yake na viongozi wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Zanzibar yamezingatiwa katika uamuzi huu," Bimani alisema.

Hata hivyo, Bimani alisema wanatambua kuwa ni lazima kuwapo na mchakato wa kupata mwafaka wa namna ya kufanikisha kupatikana kwa Katiba Mpya.

"ACT-Wazalendo tumeshawasilisha mapendekezo yetu kwa Kikosi Kazi cha Rais, tunaamini kikosi kazi kitaratibu maoni na mapendekezo ya vyama vyote na wadau wengine na kuyafikisha serikalini ili mchakato wa Katiba Mpya uanze ifikapo mwezi Oktoba kama tulivyopendekeza," alisema.

Alisema wanatarajia juhudi za kukamilisha mchakato wa kupata Katiba Mpya na Tume Huru ya Uchaguzi zitakwenda sambamba na kuharakisha maridhiano ya Zanzibar.

"Mapendekezo yetu kuhusu maridhiano ya Zanzibar yamewasilishwa kwa mamlaka zote pamoja na Kikosi Kazi cha Rais," alisema.

Mchakato wa Katiba Mpya ulisimamiwa na iliyokuwa Tume ya Marekebisho ya Katiba chini ya uenyekiti wa Jaji mstaafu Joseph Warioba, kukiandaliwa rasimu ya Katiba iliyokabidhiwa Desemba 30 mwaka 2013.

Safari ya mchakato wa kupata Katiba Mpya ilianza mwaka 2010 wakati Rais wa wakati huo, Jakaya Kikwete, alipoamua kuutangazia umma dhamira na nia ya serikali kuanzisha mchakato huo.

Mchakato ulianza rasmi mwaka 2011 kwa kutungwa kwa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Na. 83/2011 na baadaye ikatungwa Sheria nyingine ya Kura ya Maoni Na. 11/2013.

# Mbaroni akituhumiwa kuua mwanamke 'gesti'

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linamshikilia Heri Chisanga (33), mkazi wa Mburahati, kwa tuhuma za kumuua Leonia Julius (35) kwa sababu ambazo bado hazijajulikana.

Kwa mujibu wa Kamanda wa kanda hiyo, Jumanne Muliro, mtuhumiwa huyo alikamatwa Juni 21 ikiwa ni siku nne baada ya Juni 17, mwaka huu, kufanya tukio hilo na kukimbia.

Alisema baada ya mtuhumiwa kufanya tukio hilo, aliutelekeza mwili wa mwanamke huyo ndani ya chumba cha nyumba ya kulala wageni iitwayo Lavi Park iliyoko Tegeta kwa Ndevu, Kinondoni. "Mtuhumiwa huyu pamoja na marehemu waliingia kwenye nyumba hiyo ya kulala wageni, lakini baadaye Leonia alikutwa akiwa amepoteza maisha, upelelezi wa kina ulianza kufuatilia kwa kutumia utaalamu wa kipelelezi.

"Pia wataalamu wa upelelezi ambao ni kitengo kinachohusika na upelelezi wa kisayansi walifanya kazi ya ziada na baadaye ufuatiliaji huu ulifanikisha kumkamata mtuhumiwa akiwa Manzese, na chanzo halisi cha mauaji hayo bado kinachunguzwa," alisema Muliro.

# Mabeyo ataja mitihani jeshini

**Na Romana Mallya**

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi nchini, Jenerali Venance Mabeyo, ametaja milima na mabonde aliyopitia wakati wa kipindi chake cha uongozi, yakijumuisha uhalifu wa kigaidi uliojitokeza katika mikoa sita nchini.

Alibainisha hayo juzi usiku katika kipindi cha Dakika 45 kinachorushwa na kituo cha runinga cha ITV, akikiri 'mabonde' yapo na yataendelea kuwapo kulingana na mazingira na wakati.

Alisema kuwa katika kipindi chake cha uongozi, kulikuwa na mazingira fulani ambayo yalikuwa magumu.

"Kwanza, matishio yamebadilika, nchi imekabiliwa na viashiria kidogo vya ugaidi, unajua hayo ni changamoto kubwa na uje viashiria hivi tunaleta matishio yasiyo na mipaka, adui haonekani waziwazi, lakini kwa kushirikiana na wenzetu na wananchi kwa ujumla tumeweza kukabiliana na hali hiyo vizuri," alisema.

Jenerali Mabeyo alikumbusha mwaka 2017, alipoingia madarakani kulikuwa na shida mikoa tofauti na kuitaja kuwa ni Tanga (mapango ya Amboni), Mwanza (kwenye milima) na Pwani (Kibiti) ambako kote walipambana na kumaliza.

Pia alisema waliendelea eneo la kusini mwa Tanzania ambako mpaka sasa wanataka kuhakikisha mpaka wa Tanzania unakuwa salama.

"Hili bado tunaendelea nalo, kwa kweli katika kipindi hicho ni kigumu lakini tunashukuru kwa ushirikiano wa wananchi na vyombo vingine vya ulinzi na usalama tumeweza kuhimili.

"Lakini bahati mbaya kwamba majirani zetu wanakabiliwa na tishio hilo kwa kiasi kikubwa na sisi kama sehemu ya ukanda wetu huu wa SADC, tumekubaliana kwamba tuwasaidie wenzetu, tuna vikundi vyetu kule tunaendelea kupambana, tuna imani tutafanikiwa na Mwenyezi Mungu yupo nasi wakati wote," alibanisha.

Jenerali Mabeyo alisema watu hao baada ya kutoka Kibiti waliteremka kusini katika mikoa ya Mtwara, Ruvuma na wapo wananchi waliathirika maeneo la Tandahimba, Nanyamba, Mtwara Vijijini, Newala na maeneo kadhaa mengine mkoani Lindi.

Alisema wapo waliochomewa nyumba, kuharibiwa mali na baadhi ya Watanzania wametekwa na vikundi na kulazimishwa kuvuka upande wa pili kwa kubeba vifaa walivyohitaji.Alisema baada ya hilo kujitokeza, jeshi liliingia kikamilifu na kazi kubwa ilikuwa ni kuhamasisha wananchi wawape taarifa kwa sababu adui haonekani waziwazi, anapita kama mwananchi.

Alipoulizwa kama wapo Watanzania wanaotumika kwenye ugaidi, Generali Mabeyo alisema mtu anaweza kutumika bila kujua na kusisitiza kuwa kinachohitajika ni mwamko kwa wananchi.

**KIFO CHA JPM**

Jenerali Mabeyo alisema katika kipindi chake cha uongozi, kifo cha Rais John Magufuli kilikuwa sehemu ya mtihani kwake, akiwa na kauli:

"Nyie ni mashuhuda kwa mara ya kwanza tukampoteza Rais aliyekuwa madarakani, kilikuwa kipindi kigumu kidogo, lakini tulisimama kidete, kwa utulivu mzuri kama jeshi tukitimiza wajibu wetu kwa mujibu wa Katiba kuilinda nchi.

"Na hilo likapita salama na kumpokea Rais mpya ambaye tunaendelea naye, Samia Suluhu Hassan na ninaamini tunaendelea vizuri, nchi ipo salama mpaka sasa na tuna utulivu." Kuhusu utapeli nafasi za ajira kwa kutumia majina ya viongozi au fedha, alisema ni bahati mbaya kwa wale wanaotapeliwa kwa sababu jeshi linapokuwa na nafasi huzitangaza rasmi kwenye vyombo vya habari na haziuzwi.

Akifafanua mkakati wa kujenga jeshi dogo lenye zana, kiongozi huyo alisema maana yake ni kwamba kuna maeneo ambayo hawatahitaji watu bali vifaa vya kisasa na kufafanua zaidi kuwa kulingana na matishio yanayojitokeza sasa ya ugaidi, kunahitajika elimu ya kutosha.

Kuhusu wanajeshi wanaoachishwa au kuacha jeshi, Jenerali Mabeyo alisema wawapo uraiani, hufungwa na sheria ya ulinzi na kanuni zake ambapo hata akistaafu, bado inamlinda na akiikiuka kiapo chake kinamsuta.

Pia alisema jukumu la kwenda kulinda amani kwenye nchi zingine haliepukiki na Tanzania inapata manufaa mbalimbali ikiwamo kujifunza mambo kitaaluma, ushirikiano na wenzao na 'ustawi wa jamii wananeemeka'.

Alitaja mambo wanayojivunia katika miaka 60 ya jeshi hilo kuwa ni pamoja na wapigania uhuru wengi Tanzania ilikuwa ndiyo makao makuu yao, na kuwa kitovu cha ukombozi, kutoa mafunzo kwa majeshi na kusaidia dola katika majanga mbalimbali.

HABARI KITAIFA

# PM: Watakaohama kwa hiari kuendeleza ufugaji

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewahakikishia wakazi wanaohama kwa hiari yao kutoka katika eneo la Hifadhi ya Ngorongoro kuelekea kijiji cha Msomera, Handeni mkoani Tanga, kuwa hakuna shughuli zitakazosimama, wataendelea na ufugaji katika mazingira bora zaidi.

Aliyasema hayo jana wakati akiwaaga wakazi wa Ngorongoro, wanaohama kwa hiari yao kwenda kijiji cha Msomera na kupisha shughuli za uhifadhi katika eneo hilo. Hii ni awamu ya pili ya wakazi wanaohama katika eneo hilo kuelekea Msomera.

Mazungumzo hayo yamefanyika kwenye viwanja vya Ofisi Kuu ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCCA), Ngorongoro mkoani Arusha.

Waziri Mkuu ambaye ameshuhudia wakazi hao takribani 127 kutoka katika kaya 27 wakihama na kuelekea kijiji cha Msomera, amewapongeza kwa uamuzi huo na kuwahakikishia kwamba serikali itaendelea kuwapa ushirikiano.

Alisema uamuzi walioufanya wa kuhamia Msomera na kupisha shughuli za uhifadhi katika eneo la Ngorongoro ni uamuzi sahihi na kuwahakikishia kwamba hakuna shughuli zao zozote zitakazosimama, wataendelea na ufugaji kwa kuwa Msomera kuna eneo kubwa na la kutosha.

"Ninawaomba msafiri kwa amani kabisa na mioyo yenu ikunjuke. Isikilizeni serikali yenu inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan. Sasa hivi mko huru, nenda mkakae kwenye nchi yenu kwa uhuru," alisisitiza. Kwa upande wake, Mhifadhi Mkuu wa Ngorongoro, Dk. Christopher Timbuka alisema awamu ya pili ya kuwahamisha wakazi wa eneo la Ngorongoro kwa hiari ilianza Juni 20, kuhusisha kaya 27 zenye watu 127 na mifugo 488. Kaya moja kati ya hizo itahamia Karatu.

Dk. Timbuka amesema hadi sasa kaya zilizohama kwa hiari katika eneo la Ngorongoro katika awamu ya kwanza na ya pili ni 48 zenye jumla ya watu 233 na mifugo 899. Amesema utaratibu wa kuwahamisha umefanyika kwa kufuata hatua mbalimbali ikiwamo kuhakiki idadi ya watu.

Pia, hatua nyingine ni kusainisha vitabu vya fidia vya wakazi wanaohama kwa hiari awamu ya pili, kuhakiki idadi ya mifugo na kuiweka alama ili iweze kusafirishwa pamoja na kuhakiki na kutambua aina za nyumba za wakazi hao kwa ajili ya taratibu za ubomoaji.

Waziri Mkuu alitembelea eneo hilo lenye ukubwa wa kilomita za mraba 1,500 kuona maendeleo ya uwekaji wa alama kuzunguka eneo la hifadhi.

Alisema kuwa eneo hilo lina umuhimu mkubwa kwa Watanzania na hata nchi jirani. "Hii ni tunu tuliyopewa na Mwenyezi Mungu, uwapo wa wanyama ni kivutio kikubwa kwa shughuli zetu za utalii, ni muhimu tuilinde."

Alisema Watanzania hawana budi kuzingatia na kuzifuata sheria zilizowekwa. "Kila nchi ina utamaduni wake, hata wewe Mtanzania unapotoka kwenda nchi yoyote, fuata sheria za nchi hiyo."

## Rais Mwinyi awahakikishia wawekezaji amani, utulivu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali yake imeweka mkazo zaidi katika kuimarisha hali ya amani na utulivu pamoja na utawala bora ikiwa ni msingi muhimu wa maendeleo na kuimarisha imani ya wawekezaji wanaotaka kuwekeza Zanzibar.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano ulioandaliwa na Umoja wa Wafanyabiashara wa Ulaya kwa kushirikiana na Umoja wa Nchi za Ulaya, Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji kupitia Mamlaka ya Kukuza Uchumi Zanzibar (ZIPA) pamoja na Uholanzi, hafla iliyofanyika, mjini hapo.

Alisema Serikali ya Zanzibar imeendelea kutatua changamoto mbalimbali zinazojitokeza kwa kuendeleza umoja na mshikamano ikiwa ni pamoja na kuimarisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK).

Katika hotuba yake, Rais Dk. Mwinyi alitoa pongezi kwa waandaaji wa mkutano huo ambao utajadili jinsi ya kuzitumia fursa za uwekezaji Zanzibar na dira na dhamira ya serikali yake.

Alisema mkutano huo umekuja wakati muafaka na serikali imeelekeza nguvu zake katika kukuza uwekezaji na kuimarisha sekta ya utalii ikizingatiwa kwamba maeneo hayo yaliathiriwa na UVIKO-19.

Kwa upande wa uwekezaji alieleza kufarijika na hatua iliyofikiwa licha ya kuwapo kwa changamoto zilizoko ambazo zinatafutiwa ufumbuzi wa kudumu na serikali anayoiongoza.

Alisema, kwa kipindi cha miezi 19 baina ya Novemba 2020 hadi Mei 2022, jumla ya miradi 136 yenye thamani ya Dola bilioni 1.4 imewekezwa Zanzibar na inatarajiwa kutoa ajira 9,000.

Pia Zanzibar imekuwa na ushirikiano na uhusiano wa kiuchumi na biashara tangu karne nyingi zilizopita kati yake na nchi za Ulaya na kueleza kufurahishwa kutokana na uhusiano huo kuzidi kuendelezwa na wawekezaji kutoka nchi mbalimbali za Ulaya kuja kuwekeza visiwani humo.


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 190 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

GEORGE A. MATEMBELE……………………ACCUSED PERSON

To:
George A. Matembele
Plot No. 41, Block 6, Mbweni Mpiji Area,
Kinondoni Municipality, Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 30th day of June 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of May 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

Resident Magistrate Kivukoni/Kinondoni Resident magistrate court Dar es Salaam

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………

Signature……………

Qualification/Relationship

Date……………

216916301

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 177 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

ABDULRAHMAN MOHAMOUD DALMAR……………………ACCUSED PERSON

To:
Abdulrahman Mohamoud Dalmar
Plot No. 277, Block A, Buguruni Area
Ilala Municipality, Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 80 day of JUNE 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25 day of APRIL 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

Resident magistrate Kivukoni/Kinondoni Resident magistrate court Dar es Salaam

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………

Signature……………

Qualification/Relationship

Date……………

216916301

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 193 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

HUSSEIN ABDUL KARIM……………………ACCUSED PERSON

To:
Hussein Abdul Karim
Plot No. 234, Block B, Kigamboni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 30th day of June 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of May 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

Resident magistrate Kivukoni/Kinondoni Resident magistrate court Dar es Salaam

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………

Signature……………

Qualification/Relationship

Date……………

216916301

Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 182 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

MADOSHI ELISHA KADASHI……………………ACCUSED PERSON

To:
Madoshi Elisha Kadashi,
Kibululu Street, Goba Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 30th day of June 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of May 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

Resident magistrate Kivukoni/Kinondoni Resident magistrate court Dar es Salaam

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name……………

Signature……………

Qualification/Relationship

Date……………

216916301

# Spika awaweka sawa waziri, mbunge

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

SPIKA Dk. Tulia Ackson (picha-ni), ameagiza kuondolewa kwenye kumbukumbu za Bunge maneno yenye kumdhalilisha Mbunge wa Jimbo la Mlimba, Godwin Kunambi, iliyotolewa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula.

Kiongozi wa mhimili huo ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, alitoa uamuzi huo jana baada ya kupitia maelezo ya pande mbili akijielekeza kujua kama jambo linalolalamikiwa linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni.

Katika mchango wange juzi mbunge huyo aliongelea faida za kupanga na kupima ardhi kwa ajili ya kuongeza wigo wa kodi, huku akieleza kazi aliyofanya ya kupima ardhi akiwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, mfano ambao ulimuinua waziri huyo.

Wakati akichangia, waziri huyo aliomba taarifa; "Ninaomba mzungumzaji anapozungumza asitupe taarifa ambazo ndizo zinatuletea matatizo nchi hii, akiwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, tulikuwa na habari ya Manispaa ya Kinondoni kuongoza migogoro.

"Lakini sasa hivi kitaifa Dodoma inaongoza kwa dhuluma ambazo wamezifanya kwa wananchi, kwa hiyo huo sio mfano anaoweza kuutolea kama habari ya mafanikio kwenye kazi aliyoifanya," alifafanua.

Katika mwongozo wake, Mbunge huyo alisema: "Jambo hili limenipotezea heshima yangu kama mbunge, neno dhuluma ni tuhuma nzito sana, limenipotezea heshima yangu kama mbunge na wananchi wangu wa Jimbo la Mlimba na kwa kuwa neno hili limeingia kwenye kumbukumbu za bunge, mimi bado ni kijana kutakuwa na rekodi mbaya huko mbele ya yanayonihusu.

"Ninaomba mambo mawili, ninaomba mwongozo kama jambo hili linaruhusiwa na kama linaruhusiwa au haliruhusiwi ninaomba athibitishe au afute kauli hii, ili kumbukumbu za bunge kama mbunge heshima yangu imevunjika."

Spika Tulia, alisema kwa mujibu masharti ya ibara 100 ya Katiba, wabunge wana uhuru wa mawazo na majadiliano wakati wanapotekeleza majukumu yao ya kibunge.

"Masharti ya ibara hiyo yametiliwa mkazo katika kifungu cha tatu cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, kwa kuzingatia masharti ya katiba na sheria mbunge anao uhuru wa kutoa mawazo na maoni wakati wa majadiliano katika bunge.

"Uhuru huo hautahojiwa na mtu au chombo chochote katika Jamhuri au mahali popote nje ya Bunge."

Spika alisema mchango wa Kunambi ulijielekeza katika umuhimu wa kupima na kupanga ardhi nchini, ili kuhakikisha kuwa faida za matumizi bora ya ardhi zinapatikana, na alieleza alivyofanya kazi hiyo akiwa Jiji la Dodoma.

"Maneno hayo yanaingilia uhuru wa mawazo na majadiliano ya Kunambi na kama alivyolalamika maneno hayo hayaleti taswira nzuri kwa nafasi yake kama mbunge na kwa wananchi anaowawakilisha na aliowahi kuwahudumia alipokuwa Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma.


"Hayo sio maneno yanayoruhusiwa katika mijadala ya bunge kwa mujibu wa kanuni ya 71 fasili ya kwanza (i) na (j), zinazuia kumsema vibaya mbunge na matumizi yasiyo sahihi ya lugha ya kumdhalilisha mbunge.

"Haikuwa sahihi kwa waziri kutaka kuwa ilifanyika dhuluma kwa wananchi, endapo kuna dhuluma ilifanyika kuna vyombo vinavyoweza kuchunguza na kuthibitisha madai hayo na hatua stahiki zikachukuliwa.

Alisema kwa mujibu wa kanuni ya 76 maneno hayo hayaruhusiwi na haikuwa sahihi kwa waziri kuyatamka.

"Naelekeza maneno yanayolalamikiwa yafutwe kwenye kumbukumbu za bunge za Juni 21, mwaka huu, kwa mujibu wa kanuni ya 5 fasili ya 1 ya kanuni za kudumu za bunge," alisema Spika Tulia.





Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 180 OF 2021.

THE REPUBLIC

VERSUS

GLORIA MWINGIRA……………………………ACCUSED PERSON

To:
Gloria Mwingira,
Plot No. 45, Block G, Magomeni Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 30th day of June 2022 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of May 2022


RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name……………
Signature……………
Qualification/Relationship
Date……………

Resident magistrate Kivukoni/Kinondoni Resident magistrate court Dar es Salaam

216916301



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF MANYARA
(AT BABATI)

CRIMINAL CASE NO. 09 OF 2022

THE REPUBLIC

VERSUS

KIFARU OIL INVESTMENT LIMITED……………………………ACCUSED PERSON

To:
Managing Director
Kifaru Oil Investment Limited
Katesh town, Katesh District
Manyara Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSONS OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO. 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 28th day of June 2022 at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of MAY 2022.


RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

RESIDENT MAGISTRATE MANYARA

Served Upon Me/us:
Name……………
Signature……………
Qualification/Relationship
Date……………

216916301



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
(AT KINONDONI)

CRIMINAL CASE NO. 197 OF 2021

THE REPUBLIC
VERSUS

SWAHILI CERAMICS STORE LIMITED ……………1ST ACCUSED PERSON
RASHID NASSOR MOHAMED……………2ND ACCUSED PERSON
MUHAMMAD HANIF ARSALAN……………3RD ACCUSED PERSON
KHALID MUHAMMAD DIN……………4TH ACCUSED PERSON
ZAFAR MUHAMMAD DIN……………5TH ACCUSED PERSON

To:
Rashid Nassor Mohamed, Muhammad Hanif Arsalan, Khalid Muhammad Din & Zahar Muhammad Din
Directors / shareholders
Swahili Ceramics Store Limited
Plot No. 54, Chang'ombe Road, Temeke Municipality
Dar Es Salaam

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 30th day of June 2022 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.


GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of May 2022

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name……………
Signature……………
Qualification/Relationship
Date……………

216916301



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE DISTRICT MAGISTRATE'S COURT OF MBEYA
(AT MBEYA)

CRIMINAL CASE NO. 33 OF 2022

THE REPUBLIC

VERSUS

JUMANNE MOHAMED NKANA……………………………ACCUSED PERSON

To:
Jumanne Mohamed Nkana
Plot No. 489, Block F,
Iwambi Area, Mbeya City

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 28th day of June 202.. at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 2nd day of June 2022

RESIDENT MAGISTRATE

DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE MBEYA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

216916301

# Taasisi ya Ruge Mutahaba kuzinduliwa rasmi Jumapili

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Ruge Mutahaba inatarajia kuzinduliwa rasmi keshokutwa mkoani Dar es Salaam ikiwa imejikita katika mambo makuu matano ambayo ni ubunifu, uvumbuzi, umahiri, upambanaji na uzalendo. Uzinduzi wa tukio hilo utarushwa mbashara kuanzia saa tatu na robo usiku kupitia vyombo vya habari vya ITV, EATV, Clouds TV na ETV.

Akizungumza jana na waandishi wa habari kwa niaba ya familia, Rwebu Mutahaba, alisema taasisi hiyo inakuja miaka mitatu baada ya kifo cha Ruge, ili kuendeleza maono yake yaliyojikita katika ustawi wa vijana, wanawake na Tanzania kwa ujumla.

Rwebu alisema enzi za uhai wake, Ruge alijitahidi kuwekeza katika ubunifu na ujasiriamali wa vijana wanawake ili kuwasaidia kuinua kipato chao.

"Kuanzishwa kwa taaisisi hii ni mwitikio wa sauti za wananchi kutokana na nafasi kubwa aliyokuwa nayo Ruge, katika kuwakilisha na kutekeleza maono yake chanya ya kimaendeleo yaliyolenga vijana, wanawake na taifa kiujumla kwa kupitia miradi mbalimbali kama fursa," alisema.

Rwebu alisema kwa kutambua kuwa moja ya tatizo kubwa linalowakabili vijana na wanawake ambao ni asilimia kubwa ya Watanzania ni ajira, taasisi ya Ruge imetengeneza mkakati na kuendesha miradi ya kusaidia.

"Taasisi ya Ruge Mutahaba imetengeneza mkakati na kuendesha miradi ya kuwasaidia wanawake na vijana kupitia ujasiriamali wenye tija, sanaa na ubunifu.

Suma Mwaitenda ambaye ni mmoja wa viongozi wa muda mrefu wa taasisi hiyo, alisema kati ya maeneo muhimu yatakayopewa kipaumbele ni ufadhili wa masomo na ushauri wa kitaaluma kwa vijana zaidi ya 5,000 kwa mwaka na kuwaunganisha takribani 10,000 na fursa za kiuchumi.

Pia alisema watajikita kutengeneza kituo au sehemu ambayo vijana watakutana, kujadiliana matatizo yao na kuunganishwa na wadau wezeshi.

Alisema Watanzania wameombwa kushiriki katika uzinduzi wa taasisi kupitia vyombo vya habari tajwa ambavyo vitarusha tukio hilo mbashara siku ya Jumapili.

Alisema baada ya uzinduzi wataendelea kushirikiana na taasisi kwenye uendeshaji wa miradi mbalimbali.




Mwakilishi wa Familia ya Ruge Mutahaba, Rwebu Mutahaba (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana, kuhusu uzinduzi wa Taasisi ya Ruge Mutahaba, unaotarajiwa kufanyika Jumapili hii. Wengine ni Mjumbe wa Bodi ya Udhamini ya Taasisi hiyo, Georgia Mutagahywa (kushoto) na Mkurugenzi wa Mradi wa Fursa, Suma Mwaitenda. **PICHA: MARY KADOKE**

# Jiji latoa ufafanuzi wauzaji magazeti

**Na Romana Mallya**

JIJI la Dar es Salaam limetoa ufafanuzi kuhusu kilichoripotiwa dhidi ya wauzaji wa magazeti kwenye maeneo ya katikati jijini humo kuwa hakuna mamlaka yoyote iliyotoa maelekezo ya kuwaondoa.

Kauli hiyo imekuja baada ya kuwapo kwa malalamiko ya baadhi ya wafanyabiashara hao kulalamikia vitendo vya askari wa Jiji la Dar es Salaam kuwanyanyasa na kuchukua meza zao.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano, Habari na Uhusiano wa Jiji hilo, Tabu Shaibu, operesheni ya kuliweka Jiji la Dar es Salaam katika hali ya usafi kwa kaulimbiu ya 'Safisha Pendezesha Dar es Salaam' inaendelea.

"Operesheni hii inasisitiza kuwa biashara zote ni lazima zifanyike katika maeneo yaliyoruhusiwa. Kwa kutambua umuhimu wa magazeti kama chanzo cha taarifa, elimu na maarifa mbalimbali, wauzaji wa magazeti waliruhusiwa kuendelea kufanya biashara katika maeneo waliyokuwapo," alisema.

Tabu alisema hakuna mamlaka yoyote iliyotoa maelekezo ya kuwaondosha wauzaji wa magazeti.

Hata hivyo, alisema imebainika kuwa baadhi yao wamekuwa wakitumia fursa ya biashara ya magazeti kuuza bidhaa ambazo ni tofauti na magazeti, jambo ambalo haliruhusiwi.

Alisema biashara ndogo ndogo nyinginezo zilikwishatolewa maelekezo ya wapi zinapaswa kufanyika.

Alisema Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji ametoa rai kwa wauzaji wa magazeti wote kuendelea kuuza magazeti huku wakizingatia maelekezo yanayowataka kufanya biashara katika magazeti tu.

Juzi Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) lilieleza kusikitishwa na vitendo vilivyofanywa na askari wa jiji hilo vya kuwanyanyasa na kuchukua meza za wauzaji wa magazeti wanaofanya shughuli zao maeneo mbalimbali ya jijini.


Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 179 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

ADATUS KAPES....................ACCUSED PERSON

To:
Adatus Kapes,
Plot No. 3, Block 3, Mbezi Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 30 day of June 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25 day of April 20......

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name............

Signature............

Qualification/Relationship

Date............

216916301



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 186 OF 2021

THE REPUBLIC

VERSUS

LUSUBILO MWAKABIBI....................ACCUSED PERSON

To:
Lusubilo Mwakabibi
Kijitonyama Area,
Kinondoni Municipality, Dar Es Salaam

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 30th day of June 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of May 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name............

Signature............

Qualification/Relationship
Date............

Resident magistrate Kivukoni/Kinondoni Resident magistrate court Dar es Salaam

216916301



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM
*(AT KINONDONI)*

CRIMINAL CASE NO. 180 OF 2021.

THE REPUBLIC

VERSUS

GLORIA MWINGIRA....................ACCUSED PERSON

To:
Gloria Mwingira,
Plot No. 45, Block G, Magomeni Area
Kinondoni Municipality
Dar Es Salaam

**WHEREAS** your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT NO 17/1997 AS AMENDED BY SECTION 20 OF CONTRACTORS REGISTRATION (AMENDMENT) ACT NO. 15/2008

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the 30th day of June 20 22 at 08:00am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this 25th day of May 20 22

RESIDENT MAGISTRATE

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:

Name............

Signature............

Qualification/Relationship

Date............

Resident magistrate Kivukoni/Kinondoni Resident magistrate court Dar es Salaam

216916301

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wauza magazeti wapewe elimu sio kufukuzwa

**JUZI** Jukwaa la Wahariri wa Habari (TEF) lilitoa tamko la kulaani kitendo cha askari wa jiji la Dar es Salaam kuwanyanyasa na kuchukua meza za wauzaji wa magazeti wanaofanya shughuli zao maeneo mbalimbali ya jiji hilo.

Kitendo hicho kilisababisha taharuki kubwa na baadhi ya wateja wao kukosa haki yao ya kupata taarifa kupitia magazeti wanayouzwa na wafanyabiashara hao.

Katika taarifa hiyo ya TEF ilibainisha kuwa Oktoba, mwaka jana, serikali ilianza kuwaondoa wafanyabiashara wadogo pembezoni mwa barabara za jiji la Dar es Salaam, lakini wauzaji magazeti hawakuondolewa kutokana na sababu za msingi.

Kwa mujibu wa Sheria ya Ongezeko la Thamani (VAT) ya mwaka 2014, nyongeza ya 9(3) inatambua magazeti kuwa nyenzo ya elimu sio biashara.

Sheria hiyo inafanana na sheria zote za kodi na mapato na VAT duniani kote na ndiyo maana katika miji yote kuna meza za magazeti na vitabu katika kona za mitaa kwa ajili ya kuendeleza elimu na maarifa kwa watu wake.

Tunatambua kuwa uondoaji wa wafanyabiashara waliokuwa wametanda katika kila kona za barabara Jiji la Dar es Salaam, umesaidia kwa kiasi kubwa kupunguza msongamo uliosababisha hata wanaotembea kwa miguu kushindwa kupita kwenye njia walizotengewa.

Pia, baadhi ya wafanyabiashara walidiriki kugeuza vibanda vilivyojengwa kwenye vituo vya mabasi kwa ajili ya kukinga na jua, mvua wasafiri, kuwa vya kufanyia biashara ndogo ndogo na wengine kudiriki kuweka majiko ya kupikia ambayo yangeweza kusababisha hatari kwa vyombo vya moto.

Hata hivyo, jiji liliruhusu wafanyabiashara wa magazeti kuendelea kuweka meza zao ili kuwapa wateja wao haki ya kupata habari na taarifa.

Lakini, tukio la juzi la wafanyabiashara hao kutimuliwa na askari wa jiji lilisababisha sintofahamu na vyombo vya habari vinavyotegemea mauzo yanayotokana kwenye magazeti hayo kwa ajili ya kujiendesha kuingia hasara kwa bidhaa hiyo kurudi kwa wingi bila kuuzwa.

Tunajua katika kutafuta maelewano ni lazima busara ichukue nafasi yake na popote kwenye maelewano hakuna kinacho haribika.


Hivyo ni busara ikatumika elimu kuwaelimisha wafanyabiashara hao kabla ya kuchukua hatua iliyofanywa na askari hao wa jiji na kusababisha kilichojitokeza.

Jana, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ilitoa taarifa ya ufafanuzi kuhusu tukio lililotokea juzi dhidi ya wafanyabiashara hao wa magazeti ikieleza kuwa, wafanyabiashara hao waliondolewa kutokana na kuuza bidhaa nyingine zaidi ya magazeti.

Taarifa hiyo ilisema kuwa wafanyabiashara hao wanaruhusiwa kuendelea kuuza magazeti kwa kuzingatia maelekezo ya kufanya biashara ya magazeti pekee.

Tunasema taarifa hiyo ingetolewa kabla ya kuchukua hatua iliyochukuliwa ingesaidia kuondoa mtafaruku huo. Na elimu ni kitu cha msingi kwa wafanyabiashara kuelewa nini cha kufanya na nini kinatakiwa kisifanyike wanapofanya shughuli zao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

## RC iboreshe 'magenge' yaliyokuwapo kunusuru ajali zinazorejea za treni

Na Adam Fungamwango

**TUMESHUHUDIA** ajali ya treni juzi, taarifa zikisema watu wanne na wengine zaidi ya 132 wamejeruhiwa.

Kamanda wa Polisi wa Tabora, Richard Abwao, alisema jeshi hilo linaendelea kufuatilia taarifa za vifo na majeruhi kutokana na abiria wengi kukimbizwa katika Hospitali ya Mkoa wa Tabora Kitete, kwa matibabu, huku akieleza chanzo cha ajali hiyo mpaka bado hakijulikana.

Mashuhuda waliokuwapo kwenye eneo la ajali, ni kwamba ilitokea saa 5:00 asubuhi, baada ya mabehewa sita kuanguka kwenye eneo la Kilolo, Tabora.

Kwa siku za hivi karibuni tumeanza kusikia ajali za mara kwa mara za treni kitu ambacho huko nyuma hakikuwapo kabisa.

Miaka ya nyuma, ajali ya treni ilikuwa ni habari kubwa mno kama vile ya ndege kwa sababu ilikuwa haitokea hata baada ya miaka 10 za zaidi.

Wataalamu wa masuala ya usafiri duniani wanasema kuwa usafiri salama zaidi unaoshika namba moja ni ndege, halafu treni inafuatia.

Pia Tanzania ilikuwa moja ya nchi ambayo huwezi kusikia ajali za treni miaka hiyo na kuhesabiwa moja ya usafiri salama zaidi. Si kwa treni za mizigo au za abiria.

Kwa sasa hali ni kama imeanza kubadilika. Kumekuwa na ajali, ingawa si kubwa sana kama zile chache za zamani, lakini zimeanza kuongezeka na kutia wasiwasi wasafiri.

Itafika wakati sasa watu wataona ni afadhali kupanda basi kuliko treni ambao umekuwa ukiaminika zaidi ni salama na gharama ndogo. Nadhani kuna tatizo kidogo ambalo serikali kwa kushirikiana na Shirika la Reli wanapaswa kukaa chini na kuangalia changamoto hizo.

Mabehewa sita kuanguka inawezekana kwa sababu mbalimbali, ikiwamo unyevu wa eneo hilo ambalo treni hiyo iliyokuwa ikitoka Kigoma kwenda Dar es Salaam, au hata kulegea kwa nati za reli.

Sina uhakika sana na hilo kwa sababu uchunguzi unafanyika, lakini moja ya sababu ambazo huko nyuma hakukuwa na ajali sana ni kuwepo na wafanyakazi wengi pembeni mwa reli inapopita maarufu kama 'magenge'.

Hawa watu walikuwa wanahakikisha usalama wa reli kila treni inapopita. Waliishi hata maporini maeneo ambayo treni inapita, na walikuwa wakishirikiana na wanavijiji ambavyo inakatiza kuweka ushirikiano wa kulinda reli.

Ushirikiano huo ulisababisha sio magenge tu kuwa walinzi wa reli, bali hata wanavijiji nao waliungana nao kuhakikisha usalama.

Hawa walikuwa wanafanya kazi ya kukagua eneo refu la reli, kuangalia kama kuna sehemu nyevu au udongo umeporomoka, lakini hata nati kulegea, wamekuwa wakirekebisha na kusawazisha kabla ya treni kupita eneo husika salama.

Baada ya kuondolewa kwa magenge wengi kutokana na kupunguza wafanyakazi, ni kwamba usalama ya reli uko mashakani.

Si sehemu nyingi na hasa maporini ambako kuna uhakika wa usalama huo. Kutokuwapo kwa ushirikiano wa TRC na wanavijiji kupitia kwa magenge, nako kunaweza kuwafanya baadhi ya wanavijiji kushindwa hata kutoa msaada au kuripoti eneo husika kama wataona kuna hitilafu kwenye reli.

Zamani watu wengi wakiliwa na utu na ujamaa, lakini kwa sasa ambapo kila mtu anajijali mwenyewe, kumekuwa na wahalifu ambao mtu tu kwa akili yake anaweza kulegeza nati au kundi la watu kutaka kung'oa reli kutokana na biashara ya vyuma chakavu.

Hali hii inasababisha kuwepo na umuhimu tena wa kuwarudisha magenge wengi kama zamani kando ya njia za treni wa ajili ya usalama. Najua tatizo itakuwa ni kuwalipa, lakini sidhani kama TRC inapasa wawaajiri kama zamani na kuwapa nyumba, kinachotakiwa waende kisasa, wanaweza kupita vijijini vinavyopita reli na kuwatafuta vijana ambao wanaweza kufanya kazi kulinda reli kama wanavyofanya sungusungu na kuwalipa kama posho kwa jinsi watakavyokubaliana.

Hii inaweza kupunguza baadhi ya ajali zinazoweza kuzuilika, ambazo zinatokana na uhalifu wa uharibifu wa miundombinu.

Kuna ajali ambazo hutokea kwa matatizo ya kiufundi ambayo kwa treni ni nadra sana kutokea, lakini kwa hujuma kutoka kwa majahili na waharibifu wa miundombinu zitakuwa zimezuilika na kuufanya usafiri huo kuendelea kuwa salama na kuaminika.

## TANGAZO

VisionFund TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

# VISIONFUND TANZANIA MICROFINANCE BANK LTD

# CALL FOR CONSULTANCY

## INDIVIDUAL & SME LENDING MARKET RESEARCH AND CAPACITY BUILDING - TERMS OF REFERENCE

### 1. INTRODUCTION

VisionFund Tanzania Microfinance Bank Limited is a Microfinance subsidiary of World Vision which believes in brighter futures for Children, empowering communities to create incomes and jobs and unlocks economic potential for communities to THRIVE. Licensed under the Banking and Financial Institution Act 2006 VisionFund Tanzania operates in 20 Regions across the country with 52 sites. VisionFund Tanzania seeks the services of an SME/Individual lending expert to handhold the bank in the refining of products and building institutional capacity to effectively serve its customers.

### 2. OBJECTIVE

The objective of the consultation will include but not limited to:

1. Undertake market review and Competitor analysis with a view of establishing VFT competitive advantage and weakness that need to be addressed.
2. Review the current VFT products in line with market needs and competition trends and recommend changes to the existing product.
3. Review VFT structure and processes for delivering Individual and SME loans in order to developing cutting edge service delivery.
4. Uncovering new product niche within the target market that VFT can target.
5. Develop training curriculum and deliver training to appropriate staff in order to build capacity to effectively sale and manage the product. Building internal capacity through a TOT for the bank to continue with the training post the consultancy.
6. Monitoring delivery and outcome of the Training and recommend changes as needed for a period not less than 6 months.

### 3. DETAILED TASK

| Activity | Description | Time scope |
|---|---|---|
| 1.0 MARKET ASSESMENT | • Undertake Market Assessment of Microfinance operation in Tanzania- Target markets, consumer behavior patterns etc. by interviewing a minimum of 50 SME potential customers and profiling: who is the customer (annual sales, registration, # employees), and what do they need (price, product, service).<br>• Undertake Competitor analysis-that reflect the following:<br>• Size of the competitions {Competitor recent performance comparison}.<br>• Products issued by competitor including Product target market, Product pricing and product structure.<br>• Credit Operation structure. | One months- June/July 2022 |
| 2.0 PRODUCT REVIEW | • Review VFT Existing individual loan products against market need and competition.<br>• Recommend changes to the existing product.<br>• Recommend new product that VFT Can introduce to the Market. | Overlapping with previous One months- June/July 2022 |
| 3.0 MARKETING & TRAINING | • Recommend the right organizational structure for effective delivery of the Individual/ SME product.<br>• Recommend marketing strategies for different categories of VFT target market.<br>• Prepare a Marketing, credit underwriting & Customer service training TOT guide for VFT Frontline staff, taking into account the existing Loan Appraisal form and procedure.<br>• Prepare and recommend the training structure/Program for individual lending that will reflect content, frequency and who is responsible for the training.<br>• Undertake training to VFT TOT and Deliver Training to target staff alongside the trainers.<br>• Preparation of Training materials including training guides (Work Book) that will be used by ToT to deliver training to staff. | Two Months- July & August 2022 |
| 4.0 MONITORING | • Train the VFT Risk Manager and support them in monitoring the risks in the emerging SME Portfolio.<br>• Monitoring trends in new client acquisition, portfolio growth and portfolio quality and recommending to management adjustments.<br>• Monitor the effectiveness of the new process developed in delivering a cutting-edge customer service to the customers.<br>• Monitor implementation and delivery of the training as per the agreed training program. | One year- June-May 2023 |

### 4. CONSUL TANT PROFILE

The consultant who shall undertake this role must have

- Minimum of a Master's in Business administration, accounting, finance, economic or related fields.
- A minimum of ten years of professional working experience in Banking and/or Microfinance, 5 of which must be in active role in Individual Lending and SME Lending and at least three years as a consultant.
- Good writing and analytical skills, interpersonal communication and presentation skills (adult education skills), ability and desire to teach in both classroom and field settings.
- Experience working in Tanzania and/or the region is preferred.
- Sufficiently physically fit, with appropriate medical clearance.
- Writing Skills: reporting requires good computer skills including, but not limited to, working and generating reports with MS Word. Experience with PowerPoint presentations is desirable.

### 5. DELIVERABLES

The following will be the key deliverables of the consultancy:

- Inception report.
- A comprehensive Market research and competitor analysis report that shows Individual/SME market segments, unreached groups for VFT target client (target groups, Sales volumes, # of employees, Registration status, Available collateral, and positioning) and further competitive position of VFT in the Microfinance market including pricing, product adjustments, services required.
- A comprehensive VFT individual lending product & process review report and Proposed Product & Process changes including pricing, product adjustments and services required based on competitor analysis and market trends. This includes also loan forms review as necessary.
- Training material guide (Work books) for Individual/SME lending for different category of staff to be used for training, incorporating and reworking if necessary the existing loan appraisal training to match loan form.
- Training programs relating to credit underwriting to be undertaken by staff categories and timelines.
- Proposed training schedule for VFT staff across the branch network.
- Performance monitoring tools which combine growth in portfolio and clients and improvements in quality of the loan book.
- Coaching of key staff for high performance in a period not less than six months.

### 6. REQUIREMENT

VisionFund Tanzania is calling for proposals form qualified consultants. The proposal should include

- Technical approach to be used to undertake the assignment including the scope, timelines and expected output.
- Financial proposal that indicate the cost to undertake the assignment.
- Timelines for the assignment and expected date of delivery.

The proposal should reach the undersigned not later than **5 July 2022.**

**Mode of Application:**
Interested and suitably qualified firm/consultant should forward its proposal to:

**proposal@vftz.co.tz**
**OR; through the postal address below:**
**The Chief Executive Officer,**
**VisionFund Tanzania Microfinance Bank Limited,**
**P. O. Box 1546, Arusha TANZANIA.**

**Disclaimer**

VisionFund Tanzania Microfinance Bank would like to inform the general public that it has not engaged any consultant/agent to conduct recruitment on its behalf.

216916402

# TANGAZO

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **STICK UP AUCTION MART, GADAU AUCTION MART & COMPANY LIMITED, MASE INTERNATIONAL LIMITED, MUGABO AUCTION MART AND COMPANY LIMITED na MPELUKI COMPANY LIMITED** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD.** Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | STICK UP AUCTION MART | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | EDGAR PETER SILAYO | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MASHARIKI-MURIETI-ARUSHA |
| 2 | HAPPYSON M KIMARO | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | KATANINI-KINDI-MOSHI |
| 3 | PAUL A MGIMBA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | TERRAT-MADUKA KUMI-ARUSHA |
| 4 | MARIAM A OMARY | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIMINDOLOSI-OLASITI-ARUSHA |
| 5 | STEPHEN G MASSAWE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | SEURI-ARUSHA |
| 6 | PRINCIPAL PETER MBOYA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | MARIETI-ARUSHA |
| 7 | JOSEPH M MGONJA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KIMNYAKI-NGARAMTONI-ARUSHA |
| | GADAU AUCTION MART & COMPANY LIMITED | | |
| 8 | RAMADHANI J KILAZA | KIWANJA CHENYE HATI MILIKI NO.50,KITALU L NA KIWANCHA CHENYE HATI MILIKI NO.166, KITALU A, MALI YA IRENE MUSOLINI SELEMANI | KIWANJA CHA NDEGE NA MKUNDI-MOROGORO |
| 9 | ALEX N GUZUYE | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | KILONGO-MKUNDI-MOROGORO |
| 10 | DIONIZ LUCAS MALEBA | NYUMBA YENYE VYUMBA VYA BIASHARA | KIHONDA KASKAZINI-MOROGORO |
| 11 | GODFREY F MSIMBE | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | GUDUGUDU MLALI-MOROGORO |
| 12 | MOHAMED SALEHE CHILUNDA | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI | NJIA PANDA YA DUMILA-MOROGORO |
| | MASE INTERNATIONAL LIMITED | | |
| 9 | JOEL W CHUMA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KASHISHI-NYAMHONGOLO-MWANZA |
| 10 | CANTIUS T BASHARA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | KAHAMA,BUSWELU-MWANZA |
| 11 | LAZARO T MKAMA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MWANG'ALANG'A, KISESA-MAGU |
| 12 | NYEREMA M NYEREMA | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MAHINA KATI-MWANZA |
| 13 | DANIEL Y KUBEBEKA | KIWANJA CHENYE MKATABA WA MAUZIANO | ISANGIJO-KISESA-MWANZA |
| 14 | AMOS J MWAMBEPO | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | MAGAKA-KAKEBE-MWANZA |
| | MUGABO AUCTION MART AND COMPANY LIMITED | | |
| 15 | MELE N SHIMBA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI, KIWANJA NO.723,KITALU A | MAKANISANI-LAMADI |
| 16 | MARIA MTERESA MAGORI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | KABALIMU-BUNDA |
| 17 | DEOGRATIAS JAMES GWASI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI, KIWANJA N0 307,KITALU S NA GARI AINA YA PRADO LANDCRUISER YENYE NO.T915 BUP | NYASURA- BUNDA |
| 18 | KILINYA E WANZAGI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO | BUTIAMA-BUNDA |
| | MPELUKI COMPANY LIMITED | | |
| 19 | SORO O KAHINDI | NYUMBA YENYE MKATABA WA MAUZIANO INAYOMILIKIWA NA SORO O KAHINDI NA NYUMBA YA MKATABA WA MAUZIANO MALI YA MDHAMINI-EZEKIEL JOHN KINYONGE | KIROMO MAGENGENI-BAGAMOYO-PWANI |

### MASHARTI YA MNADA

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, Kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

### KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Stick up Auction Mart**
**S.L.P Arusha**
**Namba za simu:**
**0786559593**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Mugabo auction mart and company limited**
**S.L.P Mara**
**Namba za simu: 0673672848**

**NA**

**Mkurugenzi mtendaji**
**Gadau auction mart & company limited**
**S.L.P 40855 Dar Es Salaam**
**Namba za simu: 0719813030**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji.**
**Mase international limited**
**S.L.P**
**Namba za simu;**
**0710885084/ 0743885084**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Mpeluki Company limited**
**S.L.P 4391 Dar es salaam**
**Namba za simu;**
**0717457780/0787898100**

**NA**

**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Namba za simu:**
**0768790399, 0754774949**

216917002

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## MAOMBI YA TAARIFA YA KUONESHA NIA KWA AJILI YA USAMBAZAJI WA MAGARI YA KUJIPAKIA SARUJI NA KUCHANGANYA ZEGE KWA AJILI YA MRADI WA EACOP KUMBUKUMBU NA: 0010007759

EACOP Limited (Kampuni) Tanzania, kampuni ya Mafuta , inakaribisha na inaalika taasisi/kampuni zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya kusambaza Magari ya kujipakia saruji na kuchanganya zege kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Mradi wa EACOP unajumuisha ujenzi na uendeshaji wa bomba lililofukiwa chini la kusafirisha Mafuta linalokatisha mipaka ya nchi mbili na litakalo safirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Mkoa wa Tanga, Tanzania kwa ajili ya kusafirisha Mafuta katika masoko ya kimataifa. Bomba litaanzia Kabaale katika Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoa wa Tanga nchini Tanzania. Urefu wa bomba ni kilomita 1,443, kati yake kilomita 1,147 zitakuwa nchini Tanzania.

### MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

- EACOP inahitaji huduma za taasisi/kampuni zenye weledi na uzoefu kuonesha nia ya kutoa huduma ya kusambaza Magari ya kujipakia saruji na kuchanganya zege
- Aina ya magari yatakayopendekezwa yanatarajiwa kuwa na uwazo wa kupakia jumla ya saruji, mchanga, kupima kundi, kuchanganya saruji, usafirishaji, na kuiweka popote inapohitajika. Kwa hivyo ni mashine ya kusimama pekee ambayo inaweza kukamilisha kazi ya kuchanganya saruji kwa kutumia mwendeshaji mmoja mwenye uzoefu kwa mashine na kusafiri chini ya nguvu zake.
- Takriban magari tisa (9) ya kujipakia yenyewe ya kujipakia yatahitajika; hasa ya ukubwa wa aina mbili tofauti mbili yaani mita za ujazo 3.0 na uwezo wa mita za ujazo 4.5.
- Msambazaji/ wasambazaji watatakiwa kuwa na uwezo wa kutoa magari yote tisa (9) ya kujipakia ndani ya kipindi cha juu cha siku 100 za kupokea agizo
- Magari ya saruji ya kujipakia yatakodishwa na kupelekwa katika Mikoa inaypoitiwa na Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) katika mikoa nane (8) tofauti; Kagera, Tabora, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Manyara na Dodoma

### VIGEZO MUHIMU:

Kwa sababu ya ukubwa wa upeo na kusaidia kampuni zinazoonyesha nia, Mradi unahifadhi haki ya kutoa vifurushi vya kazi ya mtu binafsi na/au vifurushi vingi vya kazi kwa msambazaji anayestahiki.

Makampuni yanayovutiwa yanaweza kuingia katika makubaliano na makampuni mengine ili kuboresha uagizaji wa huduma zao hata hivyo, wote na kila mshirika katika makubaliano LAZIMA atimize mahitaji yaliyoainishwa hapa chini.

Makampuni/Mashirika yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uzoefu, utendaji na uwezo katika kutekeleza majukumu yaliyoainishwa chini ya maelezo ya huduma, kwa kiwango kikubwa nchini Tanzania, kwa kuzingatia viwango vya kitaifa na kimataifa (pamoja na Viwango vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC), wenye uzoefu wa angalau miaka 10 ya utendaji wa huduma sawa na iliyoainishwa katika upeo wa kazi.
- Uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 3.0 kwa saa pamoja na miundo mingine yenye ujazo wa mita za ujazo 4.5 kwa saa
- Uwezo wa kupewa leseni ya kusafiri barabarani nchini Tanzania
- Mfumo wa taa za barabarani
- 4x4 - Uendeshaji wa magurudumu manne, na usukani wa kaa
- Kwenye mfumo wa maji bodi ndani ya gurudumu yenye uwezo wa kuchanganya zege, pampu ya maji moja kwa ajili ya gurudumu la zege
- Gurudumu la zege yenye skrubu za kuchanganya na lenye uwezo wa kupima uzito
- Kupakua vipakuzi kwa kutumia viendelezi na uwezo wa kupima uzito
- Gurudumu la kuchanganya zege iliyofungwa yenye viwango vya ROPS na FOPS kiwango cha kwanza · Udhamini na waranti unaojumuisha masaa 2000 za kazi/ mwaka 1
- Mafunzo ya Opereta
- Seti ya huduma kwa mwaka 1 ikijumuisha matairi ya ziada
- Uwezo wa kuhudumia na kudumisha upakiaji wa magari ya saruji yanayojifunga yenyewe yenye vipuri na lori linalotembea la huduma/karakana uliomo ndani ya nchi (Tanzania.
- Mafundi waliohitimu na wenye uzoefu wa kukarabati na kutunza magari inapohitajika
- Kazi muhimu za wafanyikazi waliohitimu na uzoefu zilizoainishwa chini ya wigo wa kazi kwa miradi ya mafuta na gesi ambayo inatii mahitaji ya IFC.
- Wasilisha/Thibitisha uzoefu wa kusimamia miradi, utaratibu wa ugavi na usafirishaji vitu pamoja na manunuzi · Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuwasilisha hesabu za fedha kwa mwaka wa fedha uliopita.
- Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa katika kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi wakati wa kuwasilisha ombi la kuonesha nia.
- Utoaji wa leseni ufaao kutoka kwa mamlaka husika ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma.
- Kuzingatia Kanuni za maudhui ya Ndani za mwaka 2017 pamoja na tafsiri ya Kampuni ya Ndani na sheria za Kitaifa na Kimataifa pamoja na viwango vya Kimataifa vya mafuta na gesi.
- Thibitisha na wasilisha será za Afya, Usalama na Mazingira (HSE/OSHA) na usimamizi wa viwango vya ubora na maswala ya jamii
- Uthibitisho wa usajili katika Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Ithibati ya Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa usiozidi **MB20**) hadi kufikia saa **9:00** mchana Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **7 Julai 2022** Kichwa cha Barua Pepe ni **0010007759.**

**Muhimu:** Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).

Taarifa ya kuonesha nia iwe kwa lugha ya kiingereza.

216916101

## Vibanda vya taka vyageuzwa ofisi, maduka

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

VIBANDA vya kuhifadhia taka (ghuba), vilivyokuwa kero kwa wananchi wa Manispaa ya Shinyanga kutokana na kurundikwa uchafu kwa muda mrefu na kuhatarisha afya, vimegeuzwa matumizi na kuwa maduka na ofisi za serikali za mitaa.

Mkuu wa Idara ya Usafi na Mazingira Manispaa Shinyanga, Kuchibanda Snatus, alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake namna walivyobadilisha matumizi ya vibanda hivyo ili kuimarisha suala la usafi wa mazingira.

Alisema Manispaa ya Shinyanga kwa sasa imeweka mipango yake vizuri ya kuhakikisha mji huo unakuwa safi muda wote pamoja na kugeuza matumizi ya vibanda vya taka ambavyo vilikuwa kero kwa wananchi kutokana na kutoa harufu mbaya ya uchafu.

"Manispaa ya Shinyanga kwa sasa tumejenga dampo kubwa la uchafu hivyo hatuoni haja ya kuendelea kuwapo kwa maghuba ya kuhifadhia uchafu jirani na makazi ya watu na kwenye masoko na kwa sasa tumefunga yote na kuanza kuyageuzia matumizi na kuwa maduka na ofisi za serikali," alisema Snatus.

"Kinachofanyika katika uzoaji wa taka tumeweka mawakala watatu, ambao wanapita kila siku na magari kwenye makazi ya watu na sokoni wakikusanya uchafu na kuupeleka dampo hakuna tena mrundikano wa uchafu mji ni msafi muda wote," aliongeza.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Dome katika kata ya Ndembezi Manispaa ya Shinyanga, Solomoni Najulwa alisema mabadiliko ya matumizi ya vibanda hivyo vya taka, licha ya kumaliza kero ya uchafu umewasaidia pia kupata ofisi na kuondoka kwenye nyumba za kupanga.

Kwa upande wake, mkazi wa majengo katika manispaa hiyo, Mwanne Shabani, alisema kwa sasa wataepukana na harufu mbaya waliyokuwa wakivuta wakati vibanda hivyo vikiwapo.

Alisema awali afya zao zilikuwa hatarini kwasababu uchafu huo ulikuwa ukizagaa kwenye makazi yao hususani kipindi cha mvua.

# Vijana kuwezeshwa ufugaji kibiashara

**Na Mbaraka Kambona,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ameitaka Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na taasisi inayoshughulika na kilimo biashara (PASS), kupitia mradi wanaoutekeleza wa kunenepesha mbuzi kuhakikisha vijana wengi wanapata ujuzi huo, ili waweze kuwa na fursa pana ya ajira na kukuza uchumi wao.

Ulega alitoa maelekezo hayo katika kikao kazi cha kupata taarifa ya utekelezaji wa mradi wa kunenepesha mbuzi unaotekelezwa kwa ushirikiano na taasisi hizo mbili kilichofanyika jijini hapa.

Alisema mradi huo ni lazima ujikite kuwasaidia vijana wengi kupata ujuzi wa kufuga kibiashara na kuwawekea mfumo mzuri utakaowasaidia kuwezeshwa kifedha ili wawe na mitaji ya kutosha kuendesha biashara ya mifugo.

"Tunataka tutoe ajira kwa vijana, hivyo ni lazima kuwatengeneza vijana wengi watakaokuwa na ujuzi wa kunenepesha mifugo, sasa hivi wanaofanya unenepeshaji wapo na wanawezeshwa na benki zetu, lakini tunataka tupate vijana wengi zaidi watakaotengenezwa kupitia mradi huu, tukiweka nguvu yetu hapo vizuri naamini tutawezesha vijana wengi kujiajiri," alisema.

Vile vile, alisema sasa sekta ya mifugo inakabiliwa na changamoto kubwa ya malisho na kwamba ni muhimu wakajikita kuzalisha malisho ya mifugo ya kutosha wakati wote jambo litakalosababisha kuwa na uzito wenye thamani sokoni.

"Katika taarifa zenu nimewasikia hapa mmeeleza mambo mengi mnayotarajia kufanya kupitia mradi mnaotekeleza, ushauri wangu ni muhimu mkachagua mambo machache mtakayoweza kutekeleza vizuri awamu kwa awamu kuliko kubeba mambo mengi na mwisho wa siku msiweze kufikia malengo," alisema Ulega.

Kutokana na changamoto ya kufa kwa mifugo iliyoikumba nchi hivi karibuni, aliwataka wataalamu kuhakikisha wanatumia taaluma zao kikamilifu ili kupunguza vifo vya mifugo nchini.

Aliitaka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), kusaidia wadau wa sekta ya mifugo kwa kuandaa mipango mizuri ya biashara na kutoa mikopo nafuu kwa wafugaji ili waweze kufanya wenye tija.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani, Dk. Angelo Mwilawa, alisema kwa muda sasa viwanda vingi vya kuchakata nyama nchini vinafanya kazi chini ya uwezo na kupitia mradi huo unaotekelezwa na TALIRI kwa kushirikiana na PASS ukisimamiwa vizuri utatatua changamoto hiyo.

Mradi huo pia utashirikisha halmashauri nchini ili vijana waliopo katika maeneo hayo waweze kushirikishwa vizuri katika kujifunza unenepeshaji wa mifugo na kuboresha maisha yao.

Mradi huo wa kunenepesha mbuzi umeanzishwa mahsusi kwa lengo la kuwaanda na kuwawezesha vijana kushiriki mafunzo ya ujasiriamali kwa vitendo ili hatimaye kuwekeza kwenye ufugaji kibiashara na kuongeza fursa za ajira kupitia sekta ya mifugo nchini.



Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (kulia), akiongea katika kikao kazi cha kupata taarifa ya utekelezaji wa mradi wa kunenepesha mbuzi unaotekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na taasisi inayojishughulisha na masuala ya kilimo biashara(PASS). Kushoto ni Mkurugenzi, Idara ya Utafiti, Mafunzo na Ugani (Sekta ya Mifugo), Dk. Angelo Mwilawa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bajaji bubu zatajwa chanzo ukatili kijinsia

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UWAPO wa bajaji zisizokuwa na usajili wa kusafirisha abiria nyakati za usiku wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, umetajwa kuchangia ongezeko la matukio ya uhalifu na ukatili wa kijinsia kwa wanawake kuporwa fedha, mikoba na simu za mkononi.

Hayo yalibainishwa jana katika mkutano wa hadhara ulioitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kizwaga, katika Kata ya Nyihogo Halmashauri ya Manispaa ya Kahama wa kusikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi hususani katika sekta ya kilimo, afya, elimu na miundombinu ya barabara.

Sophia Juma, mkazi wa Nyakato alisema, wapo baadhi ya waendesha bajaji wanajihusisha na uhalifu na utekaji wa abiria wao hususani wanawake nyakati za usiku na kuwapora simu za mkononi, mikoba pamoja na fedha.

Mkazi mwingine Salome John, alisema uhalifu huo umekuwa ukifanywa na waendesha bajaji katika njia za Nyakato, Mhongolo, Mbulu, Manzese pamoja na Mhungula na unaposhindwa kutoa vitu wanavyovihitaji wanakujeruhi na wakati mwingine wanakutishia kukuingilia kimwili bila ridhaa yao.

"Tunashangaa kuona bajaji zinazosafirisha abiria hapa Kahama zinawapiga debe, na usiku ndiyo zipo nyingi na ukipata tu jua umeibiwa na kama ukiwa mbishi utanyanyaswa kijinsia na tunaiomba serikali iingilie kati suala hili na kulitatua," alisema John.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha Bajaji na pikipiki Mkoa wa Shinyanga (UDAPI), Idisam Mapamde, alisema ofisi yake inapokea malalamiko kutoka kwa abiria ya kuibiwa mali zao huku wanawake wakifanyiwa vitendo vya ukatili nyakati za usiku na baadhi ya madereva hao wasiojulikana.

Alisema, mpaka sasa wilaya ya Kahama ina jumla ya bajaji 1,100 ambazo zimesajiliwa kutoa huduma ya kusafirisha abiria, lakini uwapo wa bajaji bubu unaitia doa sekta hiyo na kuwaomba madereva hao kutoa taarifa wanaozipona bajaji zenye wapiga debe ili waweze kuziwajibisha.

Aliiomba serikali washirikiane kwa pamoja katika kuondoa bajaji hizo kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara, wa bajaji zenye kondakta nyakati za usiku na ofisi yake imeshapokea malalamiko nane ya matukio ya namna hiyo.

Kwa upande wake, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alitoa siku 14 kwa Jeshi la Polisi kuziondoa bajaji hizo barabarani ili kudhibiti vitendo hivyo na watakaobainika kuwa na babaji hizo wafikishwe mbele ya vyombo vya sheria kwa hatua zaidi.

"Kahama sio kichaka cha kufanyia uhalifu, tunataka mji huu watu wafanye biashara kwa saa 24 bila hofu yoyote, bajaji ambazo hazina namba usajili ziondolewe barabarani mara moja na tuhakikishe tunapambana na matukio ya namna hii," aliongeza Kiswaga.

Aliwataka viongozi wa vituo vya bajaji wilayani hapa kila dereva kuwa na kitambulisho maalumu ambacho kitaendana na usajili wa namba ya chombo chake ili iwe rahisi kuwatambua vyombo vya usalama vitakapofanya ukaguzi.

# Ripoti taasisi zinazosita kuhamia Dodoma yaiva

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge, George Simbachawene, amesema anatarajia kupokea ripoti ya tathmini wiki hii juu ya taasisi zinazosita kuhamia Dodoma.

Baada ya kupokea ripoti hiyo, amesema wiki ijayo atatoa tamko la nini kifanyike kwa taasisi hizo.

Simbachawene aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akitoa majibu ya nyongeza ya Mbunge wa Ukonga (CCM), Jerry Silaa.

Mbunge huyo alisema bado zipo taasisi na mashirika yanafanyia shughuli zake Dar es Salaam.

"Je, serikali haioni umuhimu wa kutenga siku maalum kwa viongozi wa wizara na makatibu wakuu Dar es Salaam kwa ajili ya mazungumzo?" Alihoji.

Akitoa msimamo huo wa serikali kuhusu kuhamishia makao makuu Dodoma, Simbachawene alisema uamuzi wa serikali umekuwapo kwenye ilani za uchaguzi kwa miaka yote pamoja na kwamba bado kuna taasisi zinasita kuhamia Dodoma.

Alisema majengo ya serikali yanaendelea kujengwa kwenye Mji wa Serikali na kuwa serikali inaelekeza fedha nyingi Dodoma kwa sasa ili kujenga makao makuu.

"Kuna watu wanaodhani Rais Samia Suluhu Hassan hapendi Dodoma, ninataka niliseme hili wazi, maneno haya ni kumsingizia Rais, na fedha nyingi inayoingia Dodoma ni kwa ajili ya kujenga makao makuu," alisema.

Aliwahakikishia wabunge kuwa Rais Samia hana makusudi yoyote ya kurejesha Makao Makuu Dar es Salaam.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji kama serikali haioni umuhimu wa kutenga siku za kutoa huduma kwenye ofisi za Dar es Salaam ili kupunguza gharama kwa wateja wanaosafiri kufuata huduma Dodoma.

Awali, Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Ummy Nderiananga, alisema pamoja na serikali kuhamishia ofisi za Makao Makuu yake Dodoma, bado huduma zote zimeendelea kupatikana Dar es Salaam kama ilivyo kwa mikoa mingine nchini.

Alisema huduma kwa umma zitaendelea kuimarishwa na kutolewa katika maeneo yote nchini ikiwamo Dar es Salaam.

Pamoja na hayo, alisema serikali inaendelea na maboresho ya mifumo ya utoaji huduma kwa umma kwa njia ya kielektroniki ili kupunguza ulazima wa wateja kusafiri au kufuata huduma hizo ofisini.

## Mbunge ataka soko la kisasa la wavuvi Ukanda wa Pwani

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Mwantumu Zodo, amehoji lini serikali itajenga soko la kisasa la wavuvi kwenye Ukanda wa Pwani.

Akijibu swali hilo jana bungeni jijini hapa, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema serikali inaendelea kuboresha na kujenga masoko ya mazao ya uvuvi katika maeneo mbalimbali nchini, ukiwamo Ukanda wa Pwani.

Alisema kwa sasa serikali inaendelea na ujenzi wa soko la samaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo kwa gharama ya Sh. bilioni 2.8.

"Awamu ya kwanza ya ujenzi huo tayari imeanza mwezi Februari, 2022 ambapo gharama iliyotumika hadi sasa ni Sh. bilioni 1.6," alisema.

Aliongeza kuwa masoko yaliyopangwa kujengwa katika Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na Soko la Samaki la Kipumbwi wilayani Pangani.

"Soko litakalogharimu Sh. bilioni 1.24 ambapo soko hilo litaambatana na ujenzi wa chumba cha ubaridi chenye uwezo wa kuhifadhi tani 40 za samaki na kusimika mtambo barafu kwa gharama ya Sh. milioni 259.1," alisema.

Vilevile, alisema kupitia programu maalum ya uchumi wa buluu na programu ya mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF), serikali imepanga kujenga masoko mapya katika maeneo ya Somanga na Kilwa Kivinje.



Wabunge wa Viti Maalumu kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salome Makamba (kushoto) na Felista Njau, wakiingia bungeni kushiriki mkutano wa saba kikao cha 50 cha Bunge la Bajeti, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Bilioni 70/- kununua vifaa tiba vituo afya

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa serikali katika mwaka wa fedha 2022/23, imetenga Sh. bilioni 69.95 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Namtumbo (CCM), Vita Kawawa.

Mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kutenga fedha kwa ajili ya kununua vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Mtakanini kilichoko Namtumbo.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema kati ya fedha hizo, Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo imetengewa Sh. milioni 450 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaa tiba katika vituo vya afya, kikiwamo Kituo cha Afya Mtakanini.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Lucy Sabu, alihoji lini serikali itapeleka vifaa tiba katika kituo cha afya cha Mwabayanda wilayani Maswa kwenye jengo la mochwari.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema kituo hicho kimekamilika na kumhakikishia mbunge kuwa ifikapo Juni 30 mwaka huu, vituo vitakuwa vimepatiwa fedha za kununua vifaa tiba ambapo kiasi cha Sh. bilioni 47.7 zimetengwa.

Mbunge wa Kilolo (CCM), Justin Nyamoga, alisema jimbo hilo lina vituo vya afya vitatu na zahanati tisa ambazo zimekamilika zaidi ya mwaka mmoja, akihoji lini vifaa tiba vitapelekwa ili vianze kufanya kazi.

Dk. Dugange akijibu swali hilo, alisema mwaka ujao wa fedha Sh. bilioni saba zimetengwa kwa ajili ya kupeleka vifaa tiba kwenye zahanati zilizokamilika kwa awamu ya kwanza ikiwamo za jimbo hilo.




**Habari zote: Augusta Njoji , DODOMA**




Tufanye hivi ili kuepuka ajali hizi

# BUFE

IJUMAA JUNI 24, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




**Kwanini kuna Sensa ya Majengo kwa mara ya kwanza nchini mwaka huu ?**

Ukurasa 12

# Siri ya Wamasai kuwa walinzi mahiri na wauza dawa mijini



Shughuli za uuzaji dawa za kienyeji zikiendelea. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Ummy Matinde, SJMC**

UNAPOTAJA kabila maarufu nchini na linadumu na kujivunia mila yake ni Wamasai ambao kiasilia wanapatikana nchini Kenya na Tanzania.

Kwa sababu ya mila zao wanazozidumisha katika mavazi yao ya asili na wanaishi karibu na mbuga nyingi, wanajulikana zaidi nchini, hadi kufika nje ya bara Afrika. Ni sehemu hata ya kuwa vivutio vya kitalii.

Baada ya Nipashe kutingwa na maswali binafsi kulikoni Wamasai na hasa waishio mijini, wametokea kuaminika daima katika kazi ya ulinzi wa majengo na rasilimali mbalimbali, iwe makazi, ofisi, maduka na taasisi mbalimbali kama vile shule na kampuni binafsi, iliamua kufanya mazungumzo maalum kupata ufafanuzi.

Kimsingi, huonekana katika nafasi muhimu na nyeti za ulinzi, maeneo mengi wakiwashuhudia kwenye lindo mandhari ya getini na ndani, wakiwa na silaha kama vile marungu na sime.

Hata hivi sasa, mfano hai ni katika mradi wa ujenzi wa reli za kisasa maarufu SGR nchini katika sehemu zake nyingi za ulinzi, ambako zina vituo vingi kupindukia, safu ya ulinzi wanapatikana Wamasai, ikiwa ni ishara ya kukubalika kwa kampuni ya wajenzi, Yepi Merkezi kutoka nchini.

Hapo ndipo kunaibuka maswali kulikoni na nini cha kipekee wanacho jamii hiyo? Hapo ndipo mazungumzo ya Nipashe yakatua kwa vijana wa Kimasai kupata ufafanzi kutoka kwa wahusika.

Kijana Paul Laizer, anasema siri ya kupendwa kwao ni kutokana na uaminifu waliokuwa nao, hata imewajengea heshima kubwa katika mandhari hayo ya kikazi.

Anasema, wao wanajuana kwamba ni adimu kumkuta Mmasai anadanganyika na rushwa kazini au ufisadi wowote kwa lengo la kujinufaisha, dhidi ya maslahi ya anakowajibikia.

Wamasai anawaeleza, ni vigumu kwao kuingia tamaa au kupokea hongo ili labda aweze kununua gari kali au nguo akisisitiza wao ni watu wa kuridhika na hali waliyo nayo.

Msisitizo wake unaangukia zaidi hoja anayoitafsiri kwamba iko tofauti na inavyoeleweka kwa wengi, umaarufu wao Wamasai uko katika ushujaa kazini, akieleza wako kipekee kulinganisha na makabila yanayofanana nao kama vile wakurya na wameru, ambao ni mahiri kivita.

Laizer anasema, kigezo cha kukubalika kwao hakiangukii ushupavu na uwezo wa namna hiyo, akieleza msingi wao: "Wamasai sisi ni watafutaji, mchana tunauza sendo' (kandambili), usiku tunalinda. Sehemu ya kulinda ndio ya kupumzikia."

Kijana wa kimasai anayejishughulisha na kazi ya ulinzi jijini Dar es Salaam, Njipai Moleni, anafafanua hilo akisema, wao wamekuwa wakitafuta fedha kwa ajili ya kununulia mifugo na pale wanapofikia malengo yao, wanarejea kijijini na kuendelea na ufugaji.

"Unajua sisi wafugaji huwezi kurithi mifugo kabla baba hajafariki. Hivyo, sasa katika kujipatia mifugo yetu wenyewe, ndio unakuta wengine tunajiingiza katika shughuli za ulinzi ili kuweza kupata fedha za kununulia mifugo ya kwetu wenyewe, kwani baada ya kupata fedha huzituma kijijini kwa ajili ya kununulia mifugo hiyo"anafafanua.

Katika biashara hiyo kundi kubwa la Wamasai huhusika na 'umachinga' wakiuza viatu vilivyotengenezwa vya ngozi, ni wataaamu wa asili yake.

Wengine wanahusika na uuzaji wa dawa za asili, kazi ambayo hufanywa na kinamama wa Kimasai na wazee.

Muundo wa maisha wa jamii ya Kimasai, japo kwa kiasi kikubwa wanapatikana zaidi kiasili nchini katika mikoa ya Arusha na Manyara, hata hivyo kutokana na kutapakaa katika ufugaji wako katika mikoa mingi kitaifa.

Kwa kiasi kikubwa ni maeneo ambako kuna mazingira rafiki kwa ufugaji ikiwamo katika mikoa ya Tanga, Morogoro, Iringa, Mbeya na Pwani.

UCHUMI

# Kwanini kuna Sensa ya Majengo kwa mara ya kwanza nchini mwaka huu ?

## •Hizi hapa faida zake zinazomgusa kila mtu

**Na Flora Wingia**

MIEZI miwili ijayo, serikali imeandaa Sensa ya Watu na Makazi kufanyika. Kimsingi, inajumuisha maeneo matatu, ambayo ni; watu na makazi, majengo, pia anwani za makazi.

Siku chache zilizopita, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, iliandaa mkutano na wahariri wa vyombo vya habari kuelezea kwa kina kuhusu Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti ijayo, tarehe 23.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angelina Mabula, akiambatana na safu ya viongozi wa wizara yake, walitoa ufafanuzi wa maswali mbalimbali kuhusiana na sekta ya Ardhi.

Hivi sasa serikali inaandaa sensa hizo, Wizara ya Ardhi ikiwa imepiga hatua kubwa ya utekelezaji wake kwa mustakabali wa taifa.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Makazi, Deogratius Kalimenze, katika mada yake kuhusu Sensa ya Majengo na Urasimishaji wa Makazi, anakumbusha kaulimbiu iliyoko mwaka huu "Sensa kwa Maendeleo, Jiandae Kuhesabiwa."

Anazifafanua sensa hizo tatu zitafanyika kwa wakati mmoja, kazi itakayochukua siku 12, ikimaanisha kuwa na dodoso la sensa ya kawaida kwa siku sita, sensa ya majengo, na sensa ya anwani ya makazi kila moja itachukua siku tatu.

Mkurugenzi Kalimenze anaeleza Sensa ya Majengo, msingi wake unatokana na Sera ya Maendeleo ya Makazi, katika ibara yake inayotaka wizara husika kuwa na taarifa za nyumba, ukuaji wa miji na vifaa vinavyotumika katika ujenzi.

Pia, inagusa taarifa za ujenzi na gharama zinazotumika kuendeleza ujenzi nchini na mchango wa serikali, sekta binafsi katika uwepo wa nyumba za makazi na matumizi yake.

Anataja lingine linajikita kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) inayoongoza nchi, ikiitaka wizara hiyo kutambua na kuandaa 'kanzi data' ya nyumba zote nchini, kwa kushirikiana na wadau, ikiimarisha uhusiano kati ya wapangaji na wamiliki majengo nchini.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Hassan Mwinyi, kuzindua nembo ya sensa ijayo, tukio lililofanyika Zanzibar, Aprili mwaka huu. **PICHA: MTANDAO.**

Ni maudhui anayotafsiri kuwa msingi unaoisukuma serikali kufanya sensa ya majengo na makazi kwa mara ya kwanza, tangu kupatikana uhuru nchini.

**FAIDA ZILIZOPO**

Mkurugenzi Kalimenze, anaorodhesha faida kadhaa za sensa ya majengo nchini, ikijumuisha kupatikana takwimu zitakazosaidia kuwapo 'kanzi data' ya majengo yote nchini, aina na matumuzi yake.

Pia anafafanua itawezesha serikali kufanya mapitio na maboresho ya sera, sheria, kanuni na programu zinazosimamia eneo husika la uendelezaji nyumba na makazi nchini.

Lingine anataja itawezesha serikali kupata taarifa za matumizi ya majengo mbalimbali nchini, idadi yake, aina za matumizi, iwe makazi, biashara au huduma mbalimbali za kijamii kama vile shule, vituo kama vile vya afya, hospitali na polisi.

Pia, anasema sensa inawezesha kujua mchango wa serikali katika upatikanaji nyumba za makazi nchini, kama inavyoainishwa katika Sera ya Maendeleo ya Makazi nchini.

Anaeleza, ujenzi wa nyumba au majengo nchini unafanywa na serikali au taasisi zake pamoja na taasisi binafsi, huku haijaeleweka kiasi kamili cha mchango wake serikali katika ujenzi wa majengo hayo.

Hapo ndipo nafasi ya Sensa ya Majengo ya mwaka huu inatarajiwa kutoa majibu ya utambuzi kamili na mchango wa serikali ulivyo.

Faida nyingine inatajwa, ni kuwezesha serikali kufanya tathmini ya kiwango cha nyumba zilizojengwa katika maeneo yaliyopangwa na uwiano wa upatikanaji huduma za jamii katika majengo hayo.

Kwa kipindi kirefu inaelezwa, takriban asilimia 70 ya wakazi wake, wanaishi katika maeneo yasiyopangwa. Hata hivyo, wizara inaweka sawa hatua iliyopo kwamba kuna programu ya urasimishaji imeshafanyika nchi nzima na kumeshuhudiwa faida nyingi.

Mkurugenzi huyo anafafanua hilo kwamba, sensa tarajiwa itawezesha kutambua kiwango cha makazi yaliyopangwa na ambazo hazijapangwa hadi sasa.

Hapo anataja faida ya kuwezeshwa serikali kutambua hali ya uendelezaji miji katika ujenzi uliopo, yakiwemo maghorofa na majengo ya kawaida.

**SENSA YA MAJENGO**

Kwenye utekelezaji wa Sensa ya Majengo, Mkurugenzi Kalimenze, anasema itatoa viashiria mbalimbali vya utekelezaji wa majengo endelevu, katika ajenda iliyoko kuelekea haja kuwa na miji jumuishi, salama, stahimilivu na endelevu katika nchi zote duniani.

Katika kutekeleza sensa hiyo, Kalimenze anasema inaelekea kutoa viashiria vyenye azma iliyopo.

Faida nyingine anaitaja ni kusaidia utafiti unaofanyika nchini, katika masuala ya nyumba na uendelezaji miliki, kukipatikana takwimu sahihi zitakazosaidia kufanya tafiti stahiki.

**MAANDALIZI YAKOJE?**

Akibainisha maandalizi ya sensa ijayo, Kalimenze anataja hatua ya kwanza ilikuwa kuandaa nyenzo, kwa maana ya madodoso na miongozo ya usimamizi wa makarani, wakufunzi kwa ajili ya kuendesha sensa hiyo ya majengo.

Anafafanua ni hatua iliyofanyika tangu Julai mwaka jana na kuendelea hadi mwezi huu kukifanyika uboreshaji wa nyenzo, hatua iliyokamilishwa baada ya kufanyika Sensa ya Majaribio na kurudiwa tena mwezi uliopita.

Anataja hatua ya pili, ni mafunzo kwa makarani waliotumika kwenye majaribio hayo, ambayo kwa mujibu wa sheria ya takwimu, hilo linatakiwa kufanyika mwaka mmoja kabla ya sensa husika kufanyika.

Hatua ya tatu anaitaja, ni kuandaa mikakati ya uelimishaji, ambayo ulizinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan, jijini Dodoma, mnamo Septemba 14, mwaka jana.

Hapo anawataja wanahabari katika wajibu wao wa kuielimisha jamii, kuhusiana na maandalizi ya sensa yenyewe.

Itakumbukwa, Sensa ya Majaribio ilifanyika kuanzia Septemba 8 hadi 19, mwaka jana na matokeo yake kuchambuliwa hata kupatikana tathmini ya nyenzo zilizotumika na ubora wake, kuwezesha upatikanaji takwimu sahihi kwa ajili ya sensa kuu ijayo ya mwezi Agosti.

Kilichofanyika baada ya Sensa ya Majaribio, ni kuandaliwa rasimu na kuorodhesha miongozo, kisha majedwali yatakayotumika kuandaa taarifa au uchambuzi wa takwimu, kutokana na sensa ya majengo.

**SENSA INAVYOSIMAMIWA**

Sensa ya makazi na ile ya anwani, inasimamiwa kwanza kwa kuwapo, kamati kuu ya kitaifa chini ya uenyekiti wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Mwenyekiti Mwenza ni Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Pia, ipo Kamati ya Ushauri Kitaifa inayoongozwa na Katibu Mkuu katika ofisi ya Waziri Mkuu, chini yake kuna ofisi za takwimu Tanzania Bara na Zanzibar; kamati za sensa za kila mkoa zikisimamiwa na wakuu wa mikoa.

Suala la uhamasishaji na mfumo wake, unasimamiwa na makamishna wa sensa wawili, kutoka Bara na Zanzibar (wanaweza kuwapo wengine)

**DODOSO NA MASWALI**

Inaelezwa, dodoso husika lina jumla ya maswali 23 na linazungumzia aina za majengo, miliki zake, sifa ilizo nazo, urefu wake, aina za 'uniti' zilizopo kama jengo linakaliwa na mtu mmoja au zaidi, hali ya ujenzi, idadi ya yaliyokamilika, pia yanayoendelea ujenzi.

Lingine ni hali ya ukaazi wake, sababu za majengo kutokamilika, ubora wake, hali ya ujenzi, mmiliki wake, aina za miliki kama vile binafsi, mashirika, za kiserikali au asasi zisizo za kiserikali.

Vilevile kuna suala la matumizi makuu ya jengo husika, hali ya upimaji, maeneo yaliko kama yamepimwa au la, nyaraka za kisheria, vifaa vilivyotumika katika ujenzi, huduma zinazopatikana, gharama za ujenzi na gharama za mapato ya ujenzi wa majengo hayo.

Mwongozo uliopo wa sensa, ni kwamba hizo ni taarifa zitakazoisaidia serikali kufanya tathmini, namna ya kuendeleza majengo nchini, huku kukiwapo viashiria vya kupima hali ya umasikini.

Kwa mfano, kuna swali linalouliza "Jengo hili ni la aina gani?" Wao mamlaka ya awali yakiwa na kigezo chake cha tathmini "Sisi tunafahamu kuna aina mbili za majengo, ambayo ni majengo ya kawaida na ya ghorofa; aina ya tatu ni jengo ambalo halijaisha ujenzi unaendelea.'

Pia, kuna swali, "Jengo hili lina sifa gani?' huku kukiwapo kigezo cha awali 'sifa za majengo tuna aina kuu tatu. Nyumba iliyo peke yake toka msingi hadi paa bila kuungana na nyingine; nyumba mbili za aina moja zimeungana na zinaishi familia mbili tofauti; nyumba safu yaani zaidi ya tatu zimeungana zinaishi familia tofauti."

Kalimenze anasema, changamoto wanazokutana nazo kwenye Sensa ya Majaribio ni kukosekana taarifa hasa kwa majengo ambayo hayajakamilika, sababu kuu ni katika maeneo yasiyo na wakazi.

Kalimenze anasema kumekuwapo mapendekezo ya wanahabari kushiriki vyema sensa hiyo, ili kuwahamasisha wananchi na wamiliki majengo yasiyokamilika, waache taarifa zao kwa wenyeviti wa serikali za mitaa.

Huko kuna miongozo mahususi kwa kazi hiyo, kupitia fomu maalum ambazo wenyeviti husika wanafahamu mjenzi katika eneo tajwa.

Taarifa katika fomu hizo inafafanuliwa inajumuisha umiliki, namba za simu na kama wana hati.

Kalimeze anaeleza, mwezi huu una mafunzo maalum ya siku 21 kwa watekelezaji mradi huo, kabla ya kutawanywa nchi nzima kwenda kufundisha makarani wote zaidi ya 200,000 watakaotumika katika sensa ijayo.


***Mwandishi wa makala hii ni mdau wa mafunzo maalum ya maandalizi hayo.***




Anna Makinda, kiongozi wa Sensa ya Watu na Makazi kitaifa, akiendelea na jukumu lake la uhamasishaji. **PICHA: MTANDAO.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tufanye hivi ili kuepuka ajali hizi






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

ZAMANI katika jamii zetu, hatukuwa na vyombo vya moto vya kusafiria, pia hatukuwa na miundombinu mizuri ya kusafiria na kusafirisha.

Jamii zilizokuwa ahueni kiuchumi zilitumia wanyama wafugwao hususan punda, kusafiri na kusafiria, huku barabara zikiwa bila lami kama tunavyoona leo.

Watu walizoea kuwa hiyo ndiyo njia ya usafiri na usafirishaji na maisha yaliendelea kama kawaida, yakiendana na miundombinu iliyokuwapo na majengo ya nyumba za udongo, miti na nyasi.

Polepole mambo yalibadilika na ndipo mtu au familia moja moja ikaanza kuonekana na baiskeli chombo kilichowashangaza watu kuona binadamu anakipanda na kinampeleka huku akiwa na mizigo.

Zikaja pikipiki, baadaye magari na ndipo pia barabara zikaanza kuwekwa lami na maisha yakaitwa ya kisasa na miji ikakua kutokana na vijiji tulivyokuwa tukiishi zamani. Hayo yakaitwa maendeleo.

Hivi sasa, suala la punda na baiskeli vimebaki kuwa vyombo vya usafiri na usafirishaji, vitumikavyo sambamba na magari, huku punda wakizidi kutumiwa vijijini kuliko mijini, ambako pikipiki ni nyingi.

Kutokana na kuongezeka makazi ya watu, sambamba na miundombinu ya barabara, tunaona madaraja yakijengwa sehemu mbalimbali katika kurahisisha mawasiliano baina ya sehemu moja na nyingine.

Dar es Salaam, ni moja ya maeneo nchini yenye miundombinu ya kisasa sana, inayojumuisha barabara, reli na madaraja na hiyo ikitokana na hadhi ya jiji lenyewe, lililopata kuwa makao makuu ya nchi kabla ya Dodoma.

Kadri miundombinu inavyoongezeka na kuboreka, ndivyo ajali inaongezeka kutokana na kasi ya magari barabarani, pia shughuli nyingi za watu majumbani na katika maeneo mengine, yanayohusika na ama kusafiri au kusafirisha.

Hebu tuchukulie mfano wa stendi kuu ya mabasi ya Magufuli pale Mbezi Luis, stendi inayohudumia mabasi yaendayo na yatokayo mikoani, mabasi mengi na kwa kweli inahudumia abiria wengi kila siku.

Watu wengi waitumiayo stendi hiyo, ni wale wa kawaida wenye uchumi wa kawaida, kwa sababu wenye uchumi mkubwa kawaida yao ni kutumia ndege kutokana na kipato chao kuwaruhusu.

Kwa maana hiyo, wapo watu watumiao mabasi ya daladala kwenda na kurudi katika stendi hiyo, hivyo kulazimika kutumia stendi ndogo ya daladala iliyoko mkabala na stendi kuu ya Magufuli. Kwa kutumia stendi hiyo ndogo ya daladala, watu hao hulazimika kukatiza barabara ya Morogoro ambayo hivi sasa ina takriban njia sita, ili kufikia stendi hiyo, huku kukikosekana namna ya kuzuia magari yapitayo katika barabara hiyo kwa kasi.

Zimekuwa zikitokea ajali nyingi katika eneo hilo kutokana na mazingira ya stendi hizo mbili, licha ya kuwapo daraja linalotaka abiria hao kulitumia, lakini baadhi yao hupuuza tu na kujikuta katika matatizo.

Kinachofanya watu hao kutotumia daraja hilo, ni madai kuwa ni shida sana kwa mtu mwenye mzigo kupanda juu ya daraja na kushuka nao, au kwa walemavu nao kupanda na kushuka daraja hilo, kwa ajili ya kufika stendi ya Magufuli.

Hali hii ikiendelea bila hadhari kuchukuliwa hapana shaka ajali zitaendelea na tutaendelea kulaumu maendeleo kutokana tu na kushindwa kutumia huduma zinazowekwa, zikiwamo hizo za madaraja zinazolenga kunusuru maisha yetu.

Hata hivyo, ipo haja ya kutazama upya hili suala la kila mahali kujenga madaraja, hata sehemu ambazo zingestahili kujengwa mahandaki, kwa maana ya watu kupita chini na si lazima wapite juu.

Inasemekana hata kabla ya ujenzi wa stendi ya Magufuli, katika upembuzi yakinifu ilipendekezwa kujengwa handaki kutoka stendi hiyo hadi stendi ya daladala, ili wananchi wapite chini ya ardhi na kuibukia stendi hizi mbili.

Lakini kama hiyo ilionekana haiwezekani, basi ilikuwapo haja ya stendi ya daladala kuhamishiwa upande wa iliko stendi ya Magufuli, ili kuchelea abiria kuvuka barabara kufuata huduma ya stendi kuu au stendi ndogo.

Hivyo, ili kuondokana na ajali hizo, ama lichimbwe handaki, stendi ndogo ihame, matuta yajengwe, vinginevyo tutaendelea kulia na ajali za barabarani Mbezi Luis. Alamsiki!

BIASHARA

# Pata simulizi na maisha ya mchinjaji anavyopambana hadi kinaeleweka

## • Kajenga nyumba, wake watatu....

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

KILA kazi ina uzuri na ubaya wake. Mtu anaweza akasimuliwa na hata kufurahia au kuhuzunika, kwani binadamu hupitia changamoto lukuki katika maisha yake ya kawaida kila siku.

Wapo watu wengi ambao wameweza kukata tamaa ya maisha kutokana na misukosuko mbalimbali, ndiyo maana waswahili wanasema |maisha ya binadamu ni safari ndefu, inahitaji uvumilivu usikate tamaa."

Mzee Kassim Ramadhan, mwenye umri wa miaka 73 mkazi wa Mahina - Mkuyuni jijini Mwanza ni Mwenyekiti wa Soko la Wauza kuku na Machinjio, katika Soko Kuu Mbugani, ana yake mengi katika fani na ajira yake ya kuchinja kuku kila kukicha.



Mzee Kassim Ramadhan (73) (kulia mwenye kibaragashia), maarufu kwa la Osama ambaye ni Mwenyekiti wa Machinjio ya Kuku na Wauzaji katika Soko kuu Mbugani jijini Mwanza, pia ni mchinjaji akiandaa kuku wa mteja kwenye jiko la maji ya moto ili anyonyolewe manyoya. **PICHA: ANTHONY GERVAS.**

Anaanza na historia yake, alizaliwa mwaka 1949 katika kijiji cha Mkinga mkoani Tanga, lakini akahamia Mwanza 1990 kutafuta maisha, nyumbani akiacha wake watatu.

Hapo anasema, kazi ya kwanza alipofika Mwanza alifanya katika hoteli kubwa akiwa sehemu ya mapokezi ya wageni, alikotumika kwa miezi sita, akilipwa mshahara wa Sh. 100,000 kwa mwezi.

Baadaye anasema aliacha kazi hiyo kwa sababu za maslahi na kuhamia kwenye biashara ya kununua samaki aina ya sato katika Soko la Kamanga, akiwa na mtaji wa Sh.200,000, ili maisha yaweze kusonga mbele.

Mzee Ramadhan anasema, wakati huo alikuwa akiishi kwenye nyumba ya kupanga, chumba na sebule akilipa kodi ya shilingi 10,000 kila mwezi.

Anasema biashara ya samaki aliifanya miezi miwili tu na akaiweka kando, akiendelea na shughuli za kuchinja kuku ambayo alihisi 'inalipa zaidi.'

Hapo anasema, aliona hali ya neema kimaisha yakaanza 'kulipa"akaamua kwenda nyumbani Tanga kuwafuata wake zake aweze kuishi nao akiwa na watoto tisa, lakini hadi sasa idadi imefika watoto 12, wa kiume kila upande ina idadi sita na wajukuu 50, watoto wawili wameshafariki dunia.

### UTAALAMU WA KUCHINJA

Anawataja walimu wake wa kuchinja kuku ni Mzee Faraji na Mzee Salum, anaowasema walishafariki dunia, wakimuacha yeye akiendelea na fani hiyo hadi sasa katika soko kuu jijini Mwanza.

Mzee Ramadhani anasimulia wakati akiendelea na kazi ya kuchinja, alitokea tajiri mmoja maarufu kwa jina la 'Samike'mwenye asili ya Kiasia, jina alilopewa na wenyeji wa kabila a Wasukuma, kutokana na kucheza ngoma zao za asili alizokuwa anazipenda sana.

Tajiri huyo alikuwa akimpa moyo wa kuendelea kuchinja kuku, ambaye alikuwa mmiliki wa hoteli iitwayo Utan hata yeye aliweza kuwa mteja wake wa kudumu kuchinjiwa vitoweo wa hotelini.

Anasimulia kuwa kwa siku aliweza kuchinja kuku kuanzia 50 hadi 100, kutokana na biashara kuchangamka zikiwamo za wateja wengine, enzi hizo kuku mmoja alinunuliwa shilingi 1,000 hadi 1,500 kulingana na ukubwa wake.

Anasema kazi hiyo amedumu nayo muda wa miaka 32 hadi sasa na amepewa jina maarufu la 'Osama' huku akisema shughuli hizo zimemtoa kwenye umaskini mkali, akajenga nyumba ya kuishi yenye vyumba sita kwa thamani ya shilingi milioni 25 zilizotokana na faida ya uchinjaji kuu.

"Ingawa kwa sasa biashara ya kuchinja kuku imedorora sana awali tulikuwa tunachinja kuanzia kuku 100 hadi 200, sababu tuko wengi na vibarua, lakini hivi sasa mimi naishia kuchinja hata kuku 10 au 20 kutwa biashara ikiwa nzuri," ' anasema.

Anabainisha kwamba, kwa siku anachinja na kupata riziki ya shilingi 5,000 hadi 10,000, pamoja na uzee wake, hivyo hawezi kuacha kazi hiyo, alishaizoea labda.

Mzee huyo anajivuna, hivi sasa wanavifaa vya kurahisishia kazi ya kutengeneza kuku, kama vile majiko ya kutumia mkaa na kuni kwa ajili ya kuchemshia maji ya kunyonyolea manyoya kuku wa mteja na baadaye kutayarisha nyama.

Vilevile mwanzoni walisumbuliwa na halmashauri ya jiji kutokana na kukosa meza za kisasa za machinjio au sehemu ya kutengenezea kuku wateja ila hivi sasa wanazo.

### CHANGAMOTO ZAO

Anasema changamoto zinazowakabili ni baadhi ya wateja wengine wanapochinjiwa kuku na kutayarishwa nyama, hukataa kwamba yule siyo aliyempa kumchinjia sababu nyama imekuwa ni kidogo ikilinganishwa na kuku aliyemletea yeye kuchinja.

"Wateja wengine wanakuja amenunua kuku wa kigeni akiwa amedanganywa na muuzaji kwamba ni wakienyeji, hapo ndipo kasheshe inaibuka, anadai umembadilishia wewe hivyo umlipe wa kienyeji vinginevyo vurugu inatokea na mteja," anasema.

Anadai mara nyingi amekutana na changamoto hizo, wakati mwingine anataja anaweza kuhudumiwa akaenda na nyama hadi nyumbani, baadaye anarudi akidai imepungua, akisema kuku wake alikuwa mkubwa huenda amemwibia nyama zingine.

Changamoto nyingine ni ya vijana wanaochinja wakidaiwa kupoteza kuku au nyama za wateja na kusababisha 'kuliamsha dude', wateja wakorofi wakitaka kulipwa kuku mkubwa wakati alikuwa mdogo.

Anasema visa na mikasa ndani ya soko, mteja anaweza kuhudumiwa vizuri, akaenda muda mfupi anamrudisha kuku akiwa amechemshwa akisema wamemwibia nyama zake wakidai " mbona zimekuwa kidogo wakati alikuwa mkubwa?"

Hapo anasimulia, hulazimika kumlipa mwingine.

Ramadhan anasema wapo wateja hawapendi kuku wake kuchinjwa na mtu ambaye hakumkabidhi yeye, akikuta hivyo yuko radhi kumkataa akadai anunuliwe mwingine, kwa sababu hamwamini aliyechinja kama ni muislam kweli.

Anasimulia ni mara nyingi amekumbwa na dhahama hizo za kulipa wateja ambazo husababisha kutopata faida, hata kama amefanya kazi kwa bidii, huku wanajitahidi makosa hayo yasiendelee kuwa yanajitokeza.

### MCHINJAJI KIJANA

Kijana Daniel Mwita ni mkazi wa Mahina jijini Mwanza, anayesema yeye ni kibarua anayelipwa kazi yake kwa kutwa na wamiliki wa machinjio kulingana na bidii alizofanya.

Anasimulia kuwa vijana vibarua wako takribani 30, kazi yao kubwa ni kutengeneza kuku za wateja baada ya kuchinjwa, wanawapitisha kwenye maji ya moto jikoni na kunyonyoa manyoya kisha kuandaa nyama iliyokatwa vipende ili kumrahisishia akifika nyumbani aweze kupika tu.

Mwita, mzaliwa wa kijijini Nyabirongo wilayani Tarime Mara, alianza shughuli hizo jijini hapa mwaka 2014, ambazo zimempatia faida akaweza kujenga nyumbaya kuishi yenye thamani ya shilingi milioni 12.

Aidha, anasimulia ameweza kununua ng'ombe sita na kuwekeza kijijini kwao wenye thamani ya Sh. milioni 2.4 pamoja na kumiliki bodoboda moja ambayo amemkabidhi mtu kuendesha na kumpelekea fedha baada ya siku sita shilingi 60,000.

Vilevile anasema, ameweza kusomesha shule watoto wake watatu kati ya watano, pamoja na kwamba malipo yake kutwa hali imechanganya analipwa shilingi 8,000 hadi 9,000.

Mwita anasema kero ya kuwa gizani katika soko hilo imeondoka, baaada ya kupata umeme, hivi sasa wanafanya kazi kuanzia asubuhi hadi saa 2.00 usiku, hivyo wateja wao wanafurahia, tofauti awali hawakuwa na nishati hiyo wakilazimika kufunga saa 12.30 jioni machinjio hayo likiwamo soko zima.

Kijana huyo anasema, malengo yake ya baadaye ni kuacha shughuli hizo, ifikapo mwaka 2025, akihamia kufanya biashara ya nafaka na bidhaa mbalimbali kama vile mchele, maharage, dengu, mafuta ya kula, ngano, sukari na sabuni.

Anasema amelenga kukusanya mtaji wa shilingi milioni 2 za kuanzia biashara yake, kwa sababu umri nao haurudi nyuma bali unasonga mbele, anajiandaa kubadilisha maisha baadaye uzeeni ili kuepuka umaskini.

Anasimulia kuwa changamoto inayowaumiza kichwa ni wakati wa sikukuu wateja wanakuwa wengi na kusababisha kuchanganya kuku au nyama ya mteja mmoja na kumpa mwingine ambaye siyo yake, hivyo kutokea varangati mwenye nayo akitaka kulipwa kuku mwingine.





## Meya awaomba ushirikiano wakuu wa idara, madiwani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

NAIBU Meya wa Jiji la Dodoma, Emmanuel Chibago, amewataka madiwani na wakuu wa idara kuendelea kusimamia miradi mbalimbli iliyopo ndani ya halmashauri hiyo kwa uaminifu ili waendelee kupata hati safi.

Chibago alitoa rai hiyo juzi kwenye mkutano maalum wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitia na kujadili taarifa ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) uliofanyika jijini hapa.

Alisema ili Halmashauri ya Jiji iendelee kupata hati safi kutoka kwa CAG, madiwani na wakuu wa idara kwenye maeneo yao ni muhimu wakaendelea na uaminifu uliosababisha kuipata hati safi kwa miaka minne mfululizo.

"Sifa hii ambayo halmashauri yetu hii tunaipata kwa kuendelea kupata hati safi, inatokana na ninyi waheshimiwa madiwani pamoja na wakuu wa idara. Hivyo, niwaombe tushirikiane katika kuhakikisha hatupotezi hati hii safi," alisema Chibago.

Alisema kuwa baadhi ya miradi imeshaanza kufanya kazi, hivyo wanatakiwa kuisimamia kwa ajili ya kukusanya mapato ambayo yataiwezesha halmashauri kunufaika zaidi.

Fredrick Magawa, Mkaguzi Hesabu za Serikali, aliwataka madiwani hao kuendelea kuwa na moyo wa uzalendo kwa ajili ya kuisimamia miradi kwa uaminifu.

Alisema kwa kushirikiana na wakuu wa idara wanatakiwa kuona kila mradi ni jukumu lao katika kuusimamia, hivyo hakuna sababu ya kuiachia na hatimaye wakaikosa hati safi.

**Fredrick Magawa, Mkaguzi Hesabu za Serikali, aliwataka madiwani hao kuendelea kuwa na moyo wa uzalendo kwa ajili ya kuisimamia miradi kwa uaminifu.**

# Serikali yamulika vikwazo vinavyokabili wajane nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

INAKADIRIWA kuwa idadi ya wajane duniani ni takribani milioni 258 huku milioni 115 wakidhulumiwa, kufanyiwa ukatili, kukabiliwa na umaskini na kutengwa na jamii.

Vilevile, katika kila wajane 10, mmoja anaishi katika umaskini uliokithiri.

Pia, Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ikikadiria kuwa idadi ya wajane nchini kwa sasa ni zaidi ya 800,000, sawa na asilimia 3.1 ya wanawake wote nchini ambao wanakadiriwa kuwa milioni 28.5 kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2019.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, alibainisha hayo juzi alipozungumza na vyombo vya habari kuhusu maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani.

"Tunatambua kwamba maadhimisho ya Siku ya Wajane Duniani ni jukwaa linalowaleta pamoja wajane na kuwapa fursa ya kushiriki na kubaini changamoto wanazokumbana nazo na hata kuimarisha ushirikiano kwa ajili ya ufumbuzi wa changamoto zinazowakabili," alisema.

Waziri huyo alisema Tanzania huadhimisha Siku ya Wajane kwa lengo la kukuza hamasa, mshikamano na uelewa ndani ya jamii ili kuacha ukiukaji wa haki za binadamu kwa wajane.

"Hivyo, kama Taifa maadhimisho haya yanatoa fursa ya pamoja katika kubaini changamoto za wajane na namna ya kukabiliana nazo katika jamii zetu," alisisitiza Dk. Gwajima.

Alisema ni jukumu la kila mtu kulinda haki za binadamu na utu wa wajane kwa mujibu wa Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Ubaguzi dhidi ya Wanawake na ule wa haki za mtoto.

"Hivyo, katika siku ya wajane duniani, kila mtu anahimizwa kuchukua hatua thabiti katika kuwezesha wanawake, kuendeleza usawa wa kijinsia na kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na kushughulikia changamoto zinazowakabili wajane pamoja na kuwalinda ili wapate haki zao," alisema.

Waziri huyo pia alisema serikali inawatambua na kuwaenzi wanawake wote pamoja na makundi maalum, wakiwamo wajane.

Alisema juhudi mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa na serikali ili kuhakikisha shida zinazowakabili wajane zinatatuliwa.

Vilevile, alisema wizara inatoa wito kwa uongozi wa mikoa yote kuimarisha ushirikiano na wajane kupitia vyama vyao ili kutambua mahitaji yao katika maeneo yao na kutafakari hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kutoa majawabu ya upatikanaji wa mahitaji yao katika familia.

"Ninawaomba viongozi wa vyama vya wajane kuripoti kwenye ofisi za serikali ili wajitambulishe wafahamike kwa ajili ya kupata ushirikiano imara zaidi," alisema.



Mkuu wa Tawi la Utawala la Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Brigedia Jenerali Hassan Mabena, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu kuongeza idadi ya wanafunzi wa kidato cha sita walioitwa kujiunga na mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# JKT waongeza idadi ya walioitwa kambini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT) limeongeza idadi ya wanafunzi wa kidato cha sita wanaotakiwa kujiunga na mafunzo ya JKT kwa mujibu wa sheria kutokana na kuwapo na mwitikio mkubwa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkuu wa Tawi la Utawala wa JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, alisema idadi ya walioitwa awamu ya kwanza na hiyo ya pili watakuwa zaidi ya 30,000 na mafunzo hayo yatafanyika ndani ya miezi mitatu.

Alisema wahitimu hao walioitwa wanatakiwa kubeba nyaraka ambazo zitawasaidia katika udahili wa vyuo vikuu ili kuepuka usumbufu wa kuvifuata nyumbani wakati mafunzo hayo yakiendelea katika kambi mbalimbali za JKT.

Alibainisha kuwa vijana wote hao wanatakiwa kuripoti katika makambi ya JKT yaliyo karibu na maeneo wanayoishi isipokuwa kambi ya JKT Makutupora iliyoko mkoani Dodoma na ile ya Kimbiji iliyoko Dar es Salaam pamoja na Ruvu JKT iliyoko mkoani Pwani ambayo inapokea wahitimu wenye ulemavu wa kuonekana kwa macho.

Aliongeza kuwa kambi hiyo ina miundombinu ya kutoa huduma kwa kundi hilo.

Brigedia Jenerali Mabena alisema vijana hao wanatakiwa kuanza kuripoti kuanzia jana hadi Juni 25 mwaka huu.

Alisema orodha ya majina ya vijana walioitwa awamu ya pili ikiwamo vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo, inapatikana katika tovuti ya JKT.



# TARI kutoa elimu kilimo maonyesho Nanenane

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) imeanza maandalizi ya teknolojia, mbegu, zana na mbinu bora za kilimo kwa ajili ya kufundishia wakulima kwenye Maonyesho ya Wakulima, maarufu Nanenane, ambayo kitaifa yatafanyika jijini Mbeya.

Timu ya watafiti wa taasisi hiyo kutoka Makao Makuu imeungana na wenzao wa Kituo cha Uyole kilichoko jijini Mbeya kuandaa teknolojia hizo katika viwanja vya John Mwakangale yatakakofanyikia maonyesho hayo kitaifa.

Watafiti hao wameanza maandalizi hayo kutokana na maelekezo ya Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ambaye aliwataka kuhakikisha teknolojia za kisasa zinaandaliwa kwenye maonyesho hayo ili wakulima wajifunze na wakazitumie kwenye uzalishaji wa mazao.

Mkurugenzi wa Uhawilishaji wa Teknolojia kutoka TARI, Juliana Mwakasendo, alisema jana kuwa baada ya kupokea maelekezo ya waziri, waliamua kupiga kambi katika Uwanja wa John Mwakangale kwa ajili ya kushughulikia vipando mbalimbali ambavyo vimeandaliwa.

Alisema kwenye maonyesho hayo, watafiti kutoka katika vituo vyote 14 vya TARI nchini watakuwapo kwa ajili ya kuhakikisha wakulima wanafundishwa mbinu bora za kilimo cha mazao kuanzia hatua za awali mpaka kwenye uhifadhi.

"Kwa hiyo, tunawashauri wakulima wote nchini kuhakikisha wanatembelea kituo chetu ili kupata mbinu za kisasa za uzalishaji wa mazao mbalimbali, wataalamu wa mazao tofauti watakuwapo hapa na watakuwa wanawafundisha wakulima," alisema Mwakasendo.

Meneje Usambazaji wa Teknolojia na Biashara wa TARI, Magreth Mchomvu, alisema taasisi hiyo ilianza kuandaa teknolojia na vipando tangu mwezi Februari mwaka huu baada ya kupata taarifa za awali kwamba mwaka huu kutakuwa na maonyesho.

Alisema walianza kwa kuandaa vipando vya mazao ambayo yanachukua muda mrefu kukomaa ili kuendana na muda wa maonyesho na mpaka sasa baadhi ya mazao hayo yameanza kukomaa na wana matumaini kwamba mpaka kufikia Agosti Mosi yatakuwa yamekomaa.

Aliwataka wakulima wa maeneo mbalimbali kuhakikisha wanatembelea maeneo hayo wakati wa maonyesho ili wajifunze mbinu za kisasa ambazo zitawasaidia kuzalisha kwa tija tofauti na walivyozoea.

"Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Bashe kwa kuyaleta maonyesho haya Mbeya kwa sababu tuna imani kwamba ukanda huu ni muhimu sana kwa uzalishaji wa mazao kitaifa na hili ndilo ghala kuu la chakula kwa nchi yetu," alisema Magreth. Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kuwa kutokana na maonyesho hayo kufanyika kitaifa Mbeya, wamefanya maandalizi makubwa tofauti na walivyokuwa wanaandaa miaka mingine na kwamba watahakikisha yanakuwa na mafanikio.

Alisema wameandaa vipando vya mazao mbalimbali na kwa kutumia teknolojia tofauti ili kuwaelekeza wakulima wakati wa maonyesho na baada ya maonyesho.

Alisema miaka ya nyuma walikuwa wanaandaa maonyesho hayo kwa ajili ya wakulima wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pekee lakini mwaka huu wameandaa kwa ajili ya nchi nzima na ndiyo maana wataalamu wa vituo vyote 14 watakuwapo.

"Teknolojia za kanda zote zitakuwapo hapa maana wataalamu wote watakuwapo hapa, wakulima wakija hapa watajifunza mbinu zote muhimu za kilimo," alisema Dk. Bucheyeki.

Mtafiti wa Afya ya Udongo kutoka kituo cha TARI Kifyulilo cha Mafinga mkoani Iringa, Emmanuel Kadogolo, alisema wakulima pia watafundishwa namna ya kupima afya ya udongo na namna ya kurejesha rutuba kwenye mashamba yao.



Viongozi mbalimbali mkoani Mbeya, wakishiriki Baraza la Biashara la Mkoa huo, jijini humo juzi. Wengine ni Meya wa Jiji hilo, Dk. Issa Mohamed (mwenye tai) na (wa pili kushoto) ni Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Raia wa Malawi mbaroni tuhuma wizi wa pikipiki

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia Blessing Mwaghogha (28), raia wa Malawi, kwa tuhuma za kukutwa na pikipiki ya wizi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Ulrich Matei, alisema jana katika mkutano na waandishi wa habari ofisini kwake, kuwa kijana huyo alikamatwa wakati wa oparesheni mbalimbali za jeshi hilo.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa Juni 21 mwaka huu wilayani Kyela katika Mpaka wa Tanzania na Malawi akiwa na pikipiki aina ya San LG ambayo inadhaniwa kuwa ya wizi.

Alidai kuwa mtuhumiwa huyo alikutwa ametoa namba za pikipiki hiyo na alipopekuliwa, alikutwa hana nyaraka ya aina yoyote ambayo inaashiria kuwa pikipiki hiyo ni mali yake.

Kamanda Matei alisema mtuhumiwa alipohojiwa, hakuwa na maelezo ya kueleweka na hivyo akakamatwa na kuwekwa ndani kwa ajili ya upelelezi zaidi kabla ya kuchukuliwa hatua zaidi za kisheria.

"Tunaendelea na upelelezi wa shauri hili na utakapokamilika, mtuhumiwa atafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria, lakini matukio ya wizi wa pikipiki yamekuwa yakiripotiwa mara kwa mara katika maeneo tofauti ya nchi yetu," alisema Matei.

Aliwataka wananchi kuendelea kushirikiana na jeshi hilo kwa kutoa taarifa za wahalifu ili kudhibiti matukio hayo ambayo yanaathiri shughuli za maendeleo ya wananchi.

Mtuhumiwa huyo amekamatwa ikiwa ni wiki mbili tangu Wakuu wa Jeshi la Polisi wa Tanzania na Malawi wakutane na kukubaliana kudhibiti uhalifu wa kuvuka mipaka ikiwamo wizi wa pikipiki na mauaji yanayofanywa na watu wanaohama nchi moja kwenda nchi nyingine.

# Kongamano la nishati na madini kufanyika Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Mkoa wa Mbeya umeandaa kongamano la uwekezaji katika sekta ya nishati na madini ambalo limepangwa kufanyika kwa siku mbili kuanzia Juni 26 mwaka huu jijini Mbeya.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake jijini hapa jana, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alisema dhumuni la kongamano hilo ni kuwakutanisha wadau mbalimbali wa nishati na madini ili kujadili kwa pamoja fursa nyingi zilizoko kwenye sekta hizo.

"Katika kongamano hilo mada mbalimbali zitatolewa na bidhaa mbalimbali zinazohusiana na sekta ya nishati na madini zitaonyeshwa ili kuonyeshana fursa zilizopo," alisema Homera.

Alisema Mkoa wa Mbeya umeamua kufanya kongamano hilo kwa vile unaamini kuwa kuna fursa nyingi kwenye sekta hizo mkoani Mbeya ambazo bado hazijatumika ipasavyo kuwanufaisha wananchi na Taifa kwa ujumla.

Alisema mkoani Mbeya una madini aina ya niobiam ambayo hutumika kutengeneza vipuri vya ndege lakini bado hajaanza kuchimbwa, akisisitiza ni mfano mmojawapo wa fursa ambazo bado hazijatumika.

"Mkoa wa Mbeya ni wa nne nchini kwa kuzalisha madini mengi aina ya dhahabu, ambapo kwa sasa unazalisha kati ya kilo 300 na 400 kwa mwezi, hivyo tutatumia kongamano hilo kukaribisha wawekezaji kuja mkoani Mbeya kuwekeza kwenye sekta ya madini," alisema Homera.

Alisema mkoa umeandaa maeneo maalum ya uchimbaji wa dhahabu ambayo yatatolewa kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza katika uchimbaji wa dhahabu.

Alisema washiriki wa kongamano hilo watafanikiwa kupata ufafanuzi wa kina kuhusu uwekezaji wa madini ikiwamo aina ya kodi zinazotozwa, upatikanaji wa soko pamoja na biashara ya madini.

Mkuu wa mkoa alisema katika miaka ya karibuni, sekta ya madini mkoani Mbeya imeboreshwa kwa kiwango kikubwa, hali ambayo imesaidia mkoa kuongeza uzalishaji wa dhahabu kutoka kilo 28 kwa mwezi miaka michache iliyopita hadi kufikia kilogramu kati ya 300 na 400 kwa mwezi.

Homera aliwakaribisha wadau wote wa madini kujitokeza kwa wingi kwenye kongamano hilo kwa lengo la kupata uelewa zaidi kuhusu uwekezaji kwenye madini lakini pia na wao watapata fursa ya kushauri au kutoa maoni yao kuhusu namna ya kuboresha zaidi uwekezaji katika sekta za nishati na madini.





## Waandishi wakumbushwa matumizi lugha sahihi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAANDISHI wa habari wametakiwa kuzingatia sheria za haki za binadamu ili kuepuka kufanya udhalilishaji pale wanapoandika au kuripoti taarifa zao kwa jamii.

Miongoni mwa sheria hizo ni kutumia lugha sahihi wanapoandika au kuripoti masuala ya udhalilishaji ili kuepuka kumdhalilisha zaidi mhusika wa tukio. Akizungumza katika mafunzo ya waandishi wa habari mjini hapo kuhusu usawa wa kijinsia, Ofisa MipangoTume ya Uchaguzi Zanzibar, Lutfia Said Haji, alisema waandishi lazima watumie lugha nzuri ili kuepuka kufanya udhalilisha ikiwamo kuzingatia majina mfano watu wenye ulemavu kuwaita majina ambayo ni kinyume na sheria.

Alisema lazima waandishi wazingatie miiko na maadili yao ya habari ili kuandika habari zilizo bora kwa mujibu wa sheria.

"Lazima mhakikishe mnafuata maadili ikiwamo kuvaa nguo zenye staha mnapokwenda kutafuta habari sehemu mbalimbali kwa sababu nyinyi ni kioo cha jamii," alisema.

Aidha, aliwataka waandishi kuandaa vipindi ambavyo vitaelimisha jamii umuhimu wa kulinda haki na usawa wa kijinsia ili kufikia usawa wa kijinsia.

Alisema vyombo vya habari vina nafasi kubwa katika jamii na kutaka viwe mstari wa mbele kukemea na kuandika habari za udhalilishaji zinazowakwaza wanawake na watoto.

Kwa upande wao baadhi ya waandishi walioshiriki mafunzo hayo, walisema ni bora kuwapo kwa dawati la kijinsia katika vyombo vya habari ili kusaidia panapotokea matukio ya udhalilishaji.

Pia walitaka kuwapo na mwongozo maalumu katika vituo vya habari unaowaongoza waandishi kuandika habari zisizoleta udhalilishaji kwa aliye dhalilishwa ambao utawaongoza waandishi utendaji wa kazi za kila siku.

Naye Mkufunzi kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (TAMWA), John Ambrose, alisema mwandishi wa habari ana haki ya kuongoza ndani ya vyombo vya habari na wakuu wa vyombo wawawezeshe ili kufikia malengo yao kuleta maendeleo na mabadiliko katika jamiii. Alisema kuwa kuboreshwe kwa mazingira ya waandishi wa habari wanawake ili kuondoa mitazamo hasi kuwa wanaume pekee ndiyo wanastahili kuongoza.

Jonh alisema kutokana na mabadiliko ya dunia ya kuwawezesha wanawake ni vyema jamii ikajikubali ili kuleta maendeleo chanya.



Watoto wa Kijiji cha Tumbe, kisiwani Pemba, wakionyesha vipaji vyao vya ubunifu wa kutengeneza magari ya kuchezea kwa kutumia magamba ya mgomba. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZAECA yaokoa mamilioni udanganyifu ofisi za umma

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MALI za serikalini zenye thamani ya Sh. 212,695,000 zimeokolewa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, mwaka 2021, zinazotokana na matumizi mabaya ya ofisi za umma na udanganyifu.

Fedha hizo zimeokolewa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) na fedha hizo kuzirejesha serikalini.

Waziri wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Utumishi na Utawala Bora, Haruna Ali Suleiman, alisema hayo katika Baraza la Wawakilishi wakati akisoma ripoti za utekelezaji wa kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi visiwani humo.

Waziri Haruna alisema uokoaji wa mali za umma ni miongoni mwa mbinu zinazopewa kipaumbele katika udhibiti wa vitendo vya rushwa.

Alisema kuwa katika kipindi hicho pia walifanikiwa kuokoa Sh. 603,572,772 fedha zilizookolewa zote ni Sh. 816,267,772 sawa na asilimia 58 ikilinganishwa na mwaka 2020 ambazo zilikuwa ni Sh. 474,331,424.

Alisema kwa kipindi cha Januari hadi Desemba, 2021 mamlaka ilipokea malalamiko yenye tuhuma 223, zikiwamo za kushawishi na kupokea rushwa, 26, rushwa katika zabuni tatu, kukwepa kodi, 13, kutumia vibaya mali, 10 na kusafirisha magendo mbili.

Alisema pia ubadhirifu wa mali na mapato, 81, matumizi mabaya ya ofisi, 66, mirathi tatu, utapeli tatu, utakatishaji fedha, moja, uvunjaji wa mkataba, mbili, rushwa katika uwakala, tatu, kudanganya mwajiri, mbili na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, sita.

Alisema katika kipindi hicho makosa yaliyochukua nafasi kubwa ni ubadhirifu wa mali na mapato na matumizi ya ofisi ikilinganishwa na makosa mengine ambayo yalifikia kwa asilimia 48.5 na matumizi mabaya ya ofisi, asilimia 39.5.

Alisema kuwa pamoja na mafanikio hayo, bado ofisi hiyo inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa wataalamu ambao ni muhimu katika kufanikisha uchunguzi wa tuhuma kubwa na mamlaka hiyo kuomba sehemu nyingine au kuwapata baada ya malipo.

Changamoto nyingine ni kukosekana kwa fungu maalumu la fedha za kuendesha taasisi, kukosekana kwa sheria ya kumlinda mtoa taarifa na wananchi kutojuwa thamani ya kutoa taarifa kwa mamlaka kupitia njia ya simu na badala yake hutumia kutolea taarifa za mzaha.

Akisoma hotuba ya kamati ya kusimamia ofisi za viongozi wakuu wa kitaifa mjumbe wa kamati hiyo Suleiman Makame Ali, alitaka kujua hatua zilizochukuliwa dhidi ya tuhuma za ubadhirifu wa mali na mapato ya serikali na matumizi mabaya ya ofisi kwa wahusika.

"Idadi ya kesi zilizofanyiwa uchunguzi ni chache sana na kiasi ya tuhuma hizi ni ndogo ukilinganisha uzito wa suala hili katika nchi yetu," alisema.

Alisema kwa kuwa mamlaka hiyo ina jukumu la kufanya uchunguzi wa tuhuma zinazohusiana na rushwa na uhujumu uchumi, utaalamu wa hali ya juu unahitajika katika uchambuzi wa taarifa, tathmini na uwasilishaji wa majalada kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ili linapofunguliwa pasiwapo na upungufu unaosababisha kesi kuondolewa.

# Mchakato kupitia sheria zilizopitwa wakati waanza

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI imesema Zanzibar ipo katika mchakato wa kuzipitia sheria zote zilizopitwa na wakati ambazo haziendani na mabadiliko ya wakati uliopo sasa ambao umeingia katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia.

Sekta ambazo zinatarajiwa kufanyiwa mapitio makubwa ya sheria zake ni ya habari na utangazaji ambazo ni za muda mrefu na kuwa kikwazo kwa watendaji wa tasnia hiyo katika kutekeleza majukumu yake katika dunia ya sasa.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, Katibu wa Tume ya kurekebishe Sheria, Kombo Mussa, alisema serikali ipo tayari kushirikiana kwa karibu na wadau wa habari Zanzibar ili kuona sheria mpya bora ya habari inayokwenda na wakati inapatikana.

Alisema kazi kubwa imefanywa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali kuona sheria ya huduma za habari inapatikana ambayo itakidhi mahitaji yaliyoko sasa katika kuwapo kwa uhuru wa kujieleza.

Alizitaja Sheria ya Usajili wa Wakala wa Habari, magazeti na vitabu namba.5 ya mwaka 1988 kama ilivyorekebishwa na Sheria ya Namba 8 ya Mwaka 1997 pamoja na Sheria ya Tume ya Utangazaji ya mwaka 1997 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2010 ni za muda mrefu na zinahitaji marekebisho yake. Alisema sheria hizo zimepitwa na wakati ni za tangu mwaka 1988, Sheria ya Magazeti licha ya kufanyiwa marekebisho mengine mwaka 1997.

"Nataka niseme kwa ufupi sheria zote mbili ile ya Magazeti pamoja na Utangazaji zimetufikia na sisi tumekubaliana kwa pamoja ni bora ziende mbele katika ngazi ya makatibu wakuu kwa kupitiwa zaidi," alisema.

Waziri wa Habari, Tabia Maulid Mwita, akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti yake kwa mwaka wa fedha 2022-2023, alisisitiza kuwapo kwa marekebisho ya sheria za zinazohusu tasnia ya habari kwa ajili ya kuimarisha na kukuza demokrasia na utawala bora.

Alisema utawala bora siku zote unazingatia kuwapo kwa uhuru wa vyombo vya habari pamoja na wananchi kujieleza kwa kutumia vyombo hivyo katika changamoto mbalimbali zinazowakabili.

"Tumeanza kupokea mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Habari na Utangazaji ambaya yametayarishwa na wadau wenyewe na sisi tupo tayari kuyafanyia kazi kwa lengo la kupata sheria zinazokwenda na wakati zitakazoimarisha uhuru wa habari nchini," alisema.

Mwita alivitaka vyombo vya habari Zanzibar kutekeleza majukumu yake huku vikijikita zaidi katika kuzingatia maadili ya tasnia hiyo ambayo ni kuandika habari zilizofanyiwa utafiti, zenye usahihi na kujenga na kuzingatia misingi ya kudumisha amani na utulivu wa taifa.

Katibu Mtendaji wa Tume ya Utangazaji ya Zanzibar, Suleiman Abdalla, alisema mchakato wa kupata Sheria mpya ya Habari Zanzibar upo katika hatua za mwisho kufikishwa katika ngazi ya juu husika ikiwamo pamoja na Makatibu Wakuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema katika marekebisho ya Sheria mpya ya habari, ukiritimba na vikwazo katika kupata habari na usajili wa vyombo vya habari zaidi magazeti sasa utafikia mwisho wake.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**GOODLUCK MGALA** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo cha **UALIMU DARAJA 'A'** chenye usajili namba **E556-0120** kilichotolewa na **CHUO CHA UALIMU VIKINDU** mwaka **2003.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha polisi .

**POLISI TAARIFA: PWA/KIB/RB/185317/2022**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No.76 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE EMAELY SHILLAH WILLY ............DECEASES**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**WITNESS SAMWEL JOSEPH AND TIMON STEPHEN EMAELY**

### GENERAL CITATION
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**All PERSON** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **27 Day of 06, 2022**

**Dated at Dodoma this 06 day of 06,2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**SHINYANGA**
**RUFAA YA MADAI NA,1 YA 2022**
**(ASILIA SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA 1/2020 LA MAHAKAMA YA WILAYA YA KISHAPU)**
**JIYENZE JIHAMBA**
**DHIDI YA**
**RAPHAEL NJILE NA MWENZAKE**
**KWA RAPHAEL NJILE NA ANTHONY NJILE**
**POPOTE MLIPO**

Unajulishwa kwamba mnano tarehe 16/08/2022 saa 3;00 asubuhi shauri lenu la rufaa ya madai limepangwa kusikilizwa dhidi yenu.

Hivyo mnaamriwa kuhudhuria siku hiyo bila kukosa na kama hamtahudhuria, rufaa hiyo itasikilizwa na kutolewa uamuzi bila nyinyi kuwepo.

Imetolewa kwa amri yangu na kupigwa chapa ya Mahakama tarehe 15/06/2022.

15/06/2022.
U.SWALLO
/NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA SHINYANGA.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATHEW ANDILILE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA NOAH** yenye usajili namba **T325 DDF.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: MTW/MSS/RB/112/191/202**

---

## KUPOTEA KWA VYETI



**FLAVIANA LADISLAUS NKUNGA** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **BMS332/45** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **MOROGORO** mwaka **1975** na cheti cha chuo cha **TABORA TEACHER'S TRAINING COLLEGE** chenye namba za usajili **63692** kozi ya **UALIMU** kilichotolewa mwaka **1979**, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa DSM/PHQ/RB/246358/2022**

---

Ujamaa Community Resource Team

EMPOWERMENT JUSTICE STEWARDSHIP

**PO Box 15111, Arusha, Tanzania**
**www.ujamaa-crt.org**

### TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI

SHIRIKA LA UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM NI SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI LINALOJISHUGHULISHA NA KUJENGA UWEZO WA JAMII KATIKA MASUALA YA UTAWALA BORA, ARDHI NA MAZINGIRA KATIKA MIKOA YA ARUSHA NA MANYARA.

SHIRIKA LINAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA LITATEKELEZA MIRADI MIPYA IPATAYO MITATU KAMA INAVYOAINISHWA HAPA CHINI KUANZIA JUNI 2022 MPAKA MWAKA 2026

1. UCRT KWA UFADHILI WA LINCOLIN PARK ZOO (LPZ) LITATEKELEZA MRADI WA "PROTECT CONNECTIVITY OF WILDLIFE CORRIDORS AND COMMUNAL GRAZING AREAS IN COMMUNITY AREAS" KATIKA WILAYA YA SIMANJIRO NA MONDULI UTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI ZA KITANZANIA 92,200,000
2. UCRT KWA UFADHILI WA TRIAS VZW ITATEKELEZA MRADI UJULIKANAO KAMA " PROMOTE AND DRIVE RESILIENT AND SUSTAINABLE ENTERPRENEURSHIP AND INFLUENCE SYSTEM CHANGES TOWARDS MORE SOCIAL JUSTICE WORLD WIDE " KATIKA WILAYA YA MONDULI UTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI ZA KITANZANIA 634,250,000
3. UCRT KWA UFADHILI KUTOKA USAID KUPITIA RESEARCH TRIANGLE INSTITUTE ITATEKELEZA MRADI UJULIKANAO KAMA "ENHANCING CONNECTIVITY AND GOVERNANCE WITHIN THE KWA KUCHINJA ECOSYSTEM IN NORTHERN TANZANIA KWA WILAYA YA MONDULI UTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI 542,973,169.00

***MIRADI HII YOTE ITATEKELEZWA KWA KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI HUSIKA PAMOJA NA VIJIJI.***

**KWA MAWASILIANO ZAIDI director@ujamaa-crt.or.tz na manager@ujamaa-crt.or.tz**

---

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie:**
**0782253676**

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Wakili wa kina Mdee atoa kauli kifuatacho

**Na Romana Mallya**

WAKILI Aliko Mwamanenge anayeongoza jopo la mawakili wa kina Halima Mdee kupinga kufutwa uanachama wa CHADEMA, amesema bado hawajachukua hatua zozote kutokana na uamuzi wa juzi wa Mahakama Kuu kuhusu shauri hilo.

Juzi, Mahakama Kuu Masijala Kuu iliyaondoa maombi ya waliokuwa wanachama 19 wa CHADEMA baada ya kubaini yana upungufu wa kisheria.

Wakili Mwamanenge alipotafutwa jana kuzungumzia hatua zinazofuata baada ya maombi yao kutupwa, alisema jana jioni walikuwa hawajachukua hatua yoyote na walikuwa wanasubiri kuteta na wateja wao.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa kina Mdee, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimesema muda mfupi baada ya mahakama hiyo kutoa uamuzi wa shauri hilo, kiliandika barua kwa Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, ili atekeleze ile barua yake ya awali waliyomwandikia.

Wabunge hao 19 wanaoongozwa na Mdee, walifungua maombi hayo mahakamani huko kuomba mahakama itoe kibali cha kufungua kesi ya kupinga mchakato uliowavua uanachama wa CHADEMA.

Pia waliomba mahakama iweke zuio la kutokuchukuliwa kwa hatua zozote dhidi yao hadi pale maombi yao ya msingi yatakapoamuliwa.

Naibu Katibu Mkuu wa CHADEMA Zanzibar, Salum Mwalimu, alipozungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam jana, alisema wajibu wao mkubwa ni kuhakikisha taarifa ya hukumu hiyo inafika kwa Spika wa Bunge.

"Tayari tumeshafanya hivyo, tumemwandikia barua jana (juzi) jioni mara baada ya hukumu na kuituma kwa barua pepe inayotumiwa na Bunge, kupitia Katibu wa Bunge kumwelezea hukumu ile na kumtaka Spika wa Bunge kutekeleza barua ya CHADEMA ya Mei 12 mwaka huu kwa mujibu wa Ibara 71 (1) kifungu kidogo (f) ya Katiba ya mwaka 1977 kama ilivyokuwa imeshauriwa na chama.

Mwalimu alisema barua hiyo ni yenye namba C/HQ/ABM/PARL/33/38 ya Juni 22 mwaka huu iliyotiwa saini na Katibu Mkuu CHADEMA, John Mnyika, na nakala kupelekwa kwa Msajili wa Vyama vya Siasa na Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa ajili ya taarifa.

## Waziri akabidhi skana za mamilioni

**Na Munir Shemweta,** TABORA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amekabidhi skana 50 zenye thamani ya Sh. milioni 880 kwa kwa ajili ya kurahisisha kubadilisha kumbukumbu za ardhi kutoka analojia kwenda kidigitali.

Dk. Mabula alikabidhi sehemu ya skana hizo jana kwa Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora, Jabir Singano, kwa niaba ya mikoa mingine wakati akiwa katika ziara yake ya siku moja katika Mkoa wa Tabora.

Skana zilizokabidhiwa zitasambazwa kwenye mikoa ya Mwanza (9), Kagera (5), Tabora (6), Songwe (7), Dodoma (9), Shinyanga (7) na Mbeya (7) ambazo zote zinapelekwa kusaidia kazi hiyo inayoendelea kwenye mikoa hiyo.

Akizungumza wakati wa kukabdhi vifaa hivyo, Dk. Mabula alisema kuwa uamuzi wa wizara yake kutoa vifaa hivyo ni kutaka kuharakisha ubadilishaji kumbukumbu za ardhi kutoka analojia kwenda kidigitali.

"Tunatarajia sasa ninyi mliokabidhiwa jukumu hili la kubadilisha kumbukumbu kwa niaba ya wengine wote nchi nzima, mtaendelea kuifanya kazi hii kwa weledi na kuongeza kasi ili tumalize na kuondokana na masuala ya mavumbi ya kwenye mafaili na tucheze na mfumo," aliagiza.

Kwa mujibu wa waziri huyo, ubadilishaji huo una maana zaidi kwenye mifumo kwa kuwa na uhalisia wa kutambua kumbukumbu ya mtu, kutokuwa na umilikishaji mara mbili, uchakataji nyaraka sambamba na kusaidia ramani kusomana.

Mkurugenzi wa Sera na Mipango Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Amos Zephania, alisema yapo majalada ya muda mrefu wakati ulimwengu umebadilika na kwa kuliona hilo Wizara ya Ardhi imeona umuhimu wa kubadilisha kumbukumbu zake kutoka analojia kwenda kidigitali ili kwenda na wakati.

"Majalada mengine ni ya miaka 30 iliyopita lakini bado yanaisha, ulimwengu umebadilika na tumebaki kama tupo karne ya 19 au 20, wizara imeona umuhimu wa kufanya zoezi la kubadilisha ramani hizi za upimaji, michoro ya mipango miji pamoja na nyaraka nyingine za umiliki kutoka analojia kwenda digitali ili kwenda na wakati," alisema Zephania.

Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Tabora, Singano, alisema vifaa vilivyokabidhiwa vitarahisisha utendaji kazi na kuelezea utaratibu uliokuwa ukitumika kwenye ofisi yake kuwa ililazimu wataalamu wengine kufanya kazi hadi usiku.

Hadi kufikia Mei 15, 2022 ubadilishaji wa michoro ya mipangomiji 5,649 yenye viwanja 1,758,424 na ramani za upimaji 31,500 zenye viwanja 598,000 katika halmashauri 38 ulikuwa umefanyika kutoka analojia kwenda digitali.

Vilevile, utambuzi wa vipande vya ardhi 52,648 katika halmashauri za Jiji la Dodoma na Manispaa ya Tabora, Shinyanga na Ilemela umekamilika.



Balozi wa Tanzania nchini Italia, Mahmoud Thabit Kombo (wapili kushoto), akiwa na wawakilishi wa Benki ya CRDB, Meneja Uhusiano Kitengo cha Diaspora, Mercy Nkini (kushoto), Meneja Mwandamizi Mawasiliano na Uhusiano, Emmanuel Kiondo (kulia) na Meneja wa Mikopo ya Nyumba, Janerose Mwombela, ambao wapo katika ziara ya nchi za Ulaya ili kuhamasisha Watanzania waishio huko kuwekeza nyumbani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Balozi kodi ahamasisha ulipaji kodi kwa wakati

**Mwaandishi Wetu,** DODOMA

BALOZI wa Kodi na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Pwani, Subira Mgalu, amewahamasisha wafanyabiashara kulipa kodi kwa wakati na kuhimiza matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki (EFD) kwa lengo la kuongeza mapato ya serikali na kuleta maendeleo ya taifa.

Akizungumza wakati wa kuhamasisha matumizi ya mashine za EFD mkoani Dodoma jana, balozi huyo wa kodi alisema serikali inategemea kodi kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kodi zinazokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kuwaletea maendeleo wananchi wake.

"Nikiwa balozi wa kodi, ninachukua fursa hii kutoa wito kwa wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kulipa kodi kwa wakati na kuhakikisha wafanyabiashara wanatoa risiti sahihi kila wanapofanya mauzo na wananchi wanadai risiti kila wanaponunua bidhaa ili serikali itekeleze jukumu lake la kuwaletea wananchi maendeleo kupitia miradi mbalimbali," alisema Balozi Subira.

Meneja Msaidizi wa TRA Mkoa wa Dodoma, Silver Rutagwelera, alisema lengo la zoezi hilo ni kutoa elimu kwa walipakodi ili watumie mashine za EFD kwa usahihi na kulipa kodi kwa wakati.

"Dhumuni lingine la zoezi hili ni kuwahamasisha walipakodi wetu kulipa kodi ya mapato awamu ya pili. Pia kampuni pamoja na wafanyabiashara binafsi wenye mauzo kuanzia Sh. milioni 100 kuwasilisha ritani za mapato za mwaka 2021 kabla ya tarehe 30 Juni, 2022," alisema Rutagwelera.

Mfanyabiashara wa vipodozi wa Barabara ya 10 mkoani hapo, Mwajuma Pius, alisema amelipokea vizuri zoezi hilo kwa sababu wanapata fursa ya kukumbushwa wajibu wao wa kutoa risiti na kulipa kodi kwa wakati.

Laurent Masanja, mfanyabiashara mwingine wa Barabara ya 10 mkoani hapa, alisema ni muhimu wafanyabiashara kushirikiana kwa pamoja kulipa kodi kwa hiari kwa kuwa kodi ndiyo inayoisaidia serikali kupeleka huduma mbalimbali za kijamii kwa wananchi.

Utoaji wa elimu kuhusu matumizi sahihi ya mashine EFD unaofanywa na TRA ni endelevu na unafanyika mikoa yote nchini ikiwa ni pamoja na kuwahamasisha wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kulipa kodi kwa hiari na kwa wakati.

# SIMBA QUEENS YATANGAZA KUMNASA KOCHA MWASIKILI

**Na Saada Akida**

MABINGWA wa LIGI Kuu ya Wanawake Tanzania, Simba Queens ya jijini Dar es Salaam wamemtambulisha rasmi Sophia Mwasikili kuwa kocha msaidizi wa timu hiyo, imefahamika.

Mwasikili, nahodha wa zamani wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), amechukuwa nafasi iliyoachwa na Matty Mseti ambaye aliondolewa katika timu hiyo kwa sababu ya makosa ya utovu wa nidhamu.

Taarifa kutoka Simba Queens zinasema Mwasiliki amesaini mkataba wa miaka miwili na atakuwa chini ya Kocha Mkuu, Sebastian Nkoma.

Simba Queens inaendelea kuimarisha kikosi chake ikiwa ni siku chake baada ya kutangaza kuwasajili nyota wawili wapya, kiungo mkabaji kutoka Gaspo FC ya Kenya, Vivian Corozone Aquino na Zainabu Ally wa Baobab Queens ya Dodoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya alisema wanaamini Mwasikili atashirikiana vyema na Nkoma kwa ajili ya kuendelea walipoishia katika msimu huu uliomalizika kwa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Makanya alisema wameongeza nguvu ndani ya benchi hilo kwa kumchukua beki huyo wa zamani wa Twiga Stars kwa sababu ya kuhakikisha Nkoma anapata mtu sahihi wa kumsaidia ambaye anajua vizuri soka la wanawake na wachezaji wakike.

"Sofia Mwasikili ni kocha wetu mpya msaidizi na atashirikiana kocha Mkuu Nkoma kwa ajili ya kufanya vizuri na bado tunaendelea kufanya maboresho katika kikosi cha timu yetu kwa kufanya usajili katika nafasi zilizopendekezewa na benchi la ufundi," alisema na aliongeza.

"Tumeshatambulisha wachezaji wawili Vivian na Zainab lakini bado usajili unaendelea kwa ajili ya kuimarisha kikosi chetu, kambi tunatarajia kuweka kuanzia Juni 30, mwaka huu na kuanza mazoezi Julai Mosi," alisema Makanya.

Aliongeza wanatarajia kuweka kambi wiki mbili jijini Dar es Salaam baada ya hapo wanaenda Dodoma kwa ajili ya bonanza lililoandaliwa na Fountain Gate, kucheza baadhi ya mechi kwa ajili ya mechi za kirafiki kujiandaa na michuano ya Ligi ya Mabingwa kwa Wanawake ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA), itakayofanyika jijini Arusha, baadaye mwaka huu baada ya Tanzania kuthibitisha kuwa mwenyeji wa michuano hiyo.



Baadhi ya waendesha baiskeli wanaotarajiwa kushiriki kampeni ya GGML Kili Challenge kwa kupanda Mlima Kilimanjaro ikiwa na lengo la kukusanya fedha za kutunisha mfuko wa kutokomeza maambukizi ya VVU na Ukimwi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kili Challenge 2022 yanukia

**Na Mwandishi Wetu**

MASHINDANO ya Kili Challenge 2022 yanayoratibiwa na Kampuni ya Geita Gold Mine (GGML) yanatarajia kutimua vumbi kuanzia Julai 15 mwaka huu yakianzia geti la Machame na kuhitimishwa katika geti la Mweka ifikapo Julai 21.

Meneja wa Kilimanjaro Challenge Against HIV and AIDS Trust, Manace Ndoroma, aliliambia gazeti hili mashindano hayo yamepiga hatua kubwa tangu kuanzishwa kwake mwaka 2002 hadi kuwa mashindano ya kimataifa yenye kushirikisha zaidi ya wapanda mlima 500 kutoka mabara sita huku yakikusanya zaidi ya Dola milioni mbili za Marekani.

"Wewe pia unaweza kujiunga na timu yetu ya wapanda farasi na wapanda baiskeli kwa mwaka huu 2022 ili kutusaidia kuchangisha pesa. Unaweza kuona namna ambavyo kiasi kidogo utakachochangia kinavyoweza kubadilisha maisha ya mtu mwingine.

Aliongeza, "athari za VVU/Ukimwi kwa Watanzania bado ni mbaya kwani wazee wengi masikini wanalazimika kuwalea watoto wadogo baada ya kufiwa na wazazi wao kutokana na ugonjwa huu. Familia hizi nyingi hazina uwezo wa kifedha wa kuwategemeza watoto hawa, na nyingi zimeachwa bila chakula, maji au matibabu," alisema Ndoroma.

Aliongeza fedha hizo zilisaidia kuongeza ufikiaji wa huduma za kupima, kutibu, na ushauri kwa watu walioambukizwa na jamii zao.

Mwaka 2002, AngloGold Ashanti - Geita Gold Mine ilizindua mashindano hayo kwa ushirikiano na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS).

Mashindano ya Kili Challenge hufanyika kila mwaka kwa kuchangisha fedha ili kusaidia mpango wa serikali wa kutokomeza maambukizi mapya ya VVU, unyanyapaa na ubaguzi na vifo vinavyohusiana na Ukimwi.

## Coastal yamwinda straika wa Benin

**Na Cheji Bakari, TANGA**

KLABU ya Coastal Union imeweka wazi iko katika mchakato wa kumsajili straika mpya, Olatoundji Djibril ambaye ni raia wa Benin.

Mwenyekiti wa Coastal Union, Steven Mnguto ndiye aliyeanza kusimamia mchakato wa usajili wa mchezaji huyo lakini zoezi hilo litamalizwa na Kamati ya Usajili ya klabu hiyo.

" Unajua hiki ni kipindi cha tetesi za usajili, ni kweli yule mchezaji alifanya mazungumzo ya awali na mwenyekiti wa klabu, lakini bado hatujafikiana uamuzi kutokana suala zima lipo chini ya kamati ya usajili iliyoko chini ya mwenyekiti Hemed Hillary na katibu wake, Juma Mgunda," Msemaji wa Coastal Union, Miraji Wandi alisema.

Ameongeza: "Pia bado hatujafikiana atasaini mkataba wa muda gani, malipo na mambo mengine, muda wa dirisha la usajili ukifika tutangaza wachezaji wote tutakaowasajili ila kwa sasa hatuwezi kufanya hivyo kutokana kuna wachezaji wengine bado wanazitumikia timu zao, tukitangaza mapema halitakuwa jambo zuri."

Coastal Union itamaliza msimu huu wa 2021/2022 kwa kuwakaribisha Geita Gold FC kutoka mkoani Geita.

## Baseball waandaa mafunzo Julai 30

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Base Ball na Soft Ball Tanzania (TaBSA) kinatarajia kufanya semina ya mchezo huo itakayofanyika Julai 30 na 31, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Katibu Mkuu wa TaBSA, Alpherio Nchimbi alisema semina hiyo itaendeshwa na wakufunzi wa kimataifa kutoka Japan.

Nchimbi alisema lengo la semina hiyo ni kuwaongezea uwezo makocha na wachezaji wa hapa nchini kuufahamu vyema mchezo huo.

"Tunatarajia kufanya semina mwezi ujao naamini itawasaidia viongozi pamoja na wachezaji kufahamu zaidi kanuni na taratibu za mchezo huu ambao kwa sasa unazidi kukua," alisema Nchimbi.

Wakati huo huo, Nchimbi alisema kwa sasa amewapa wachezaji wake likizo huku akiweka wazi kupitia mashindano ya Kombe la Fakuoka yaliyoshirikisha vijana wenye umri chini ya miaka 12 kutoka katika shule za msingi amegundua vipaji vingi.

## ZISIKUPITE

### ANTONY AITAMANI UNITED
MSHAMBULIAJI wa Ajax na Timu ya Taifa ya Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 22, 'amedhamiria' kujiunga na Manchester United msimu huu wa joto. ***(Goal)***

### WILLIAMS KUWEKWA SOKONI
MLINZI wa pembeni wa Manchester United, Brandon Williams mwenye umri wa miaka 21, anaweza kuuzwa kwa pauni milioni 10. ***(Sun)***

### SPURS KUIKAMUA AJAX
KLABU ya Ajax inatazamiwa kuwasilisha ofa nyingine kwa winga wa Tottenham Hotspur na Uholanzi, Steven Bergwijn mwenye umri wa miaka 24, lakini klabu hiyo ya Ligi Kuu England haitakubali chochote chini ya pauni milioni 25. ***(Sky Sports)***

### WARD-PROWSE AGEUKA LULU
KLABU ya Southampton imejaribu kuzuia nia ya Manchester City, Manchester United, Tottenham Hotspur na West Ham kumnunua kiungo wa kati wa England, James Ward-Prowse mwenye umri wa miaka 27, kwa dau la pauni milioni 75. ***(Give Me Sport)***

### KAHN AMTAJA LEWANDOWSKI
OFISA Mtendaji Mkuu wa Bayern Munich, Oliver Kahn amesema anatarajia fowadi wa Timu ya Taifa ya Poland, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33, kubaki kwa mabingwa hao wa Ujerumani msimu huu wa joto. ***(Sky Sports)***

### CUCURELLA ANUKIA CITY
KLABU ya Manchester City ipo kwenye mazungumzo ya juu zaidi ya kutaka kumsajili beki wa Brighton na Timu ya Taifa ya Hispania, Marc Cucurella mwenye umri wa miaka 23. ***(Football Insider)***

### XAVI AMKUBALI DEMBELE
KOCHA wa Barcelona, Xavi anamsihi winga wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 25, kusaini mkataba mpya huku Chelsea ikimwinda. ***(Goal)***

### GAKPO KUMRITHI RAPHINHA
LEEDS United inatarajiwa kumsajili winga wa PSV Eindhoven na Uholanzi, Cody Gakpo mwenye umri wa miaka 23, msimu huu wa joto kama mbadala wa fowadi wa Brazil, Raphinha (25), ambaye analengwa na Arsenal. ***(Foot Mercato)***

### ARRIZABALAGA ANUKIA NICE
KLABU ya Nice wanamtaka kwa mkopo golikipa wa Chelsea, Kepa Arrizabalaga mwenye umri wa miaka 27. ***(Foot Mercato)***

### BROJA AKARIBIA WEST HAM
MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 20, atakuwa tayari kuhamia West Ham kwa dau la pauni milioni 25. ***(Express)***

### LUKAKU AMSUBIRISHA STERLING
CHELSEA inamngoja mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku mwenye umri wa miaka 29, kukamilisha uhamisho wake wa mkopo kwenda Inter Milan kabla ya kushughulikia nia yao ya kumnunua fowadi wa Manchester City na England, Raheem Sterling (27). ***(Sky Sports)***

### MUNETSI ATAJWA BRIGHTON
KIUNGO wa kati wa Reims na Zimbabwe, Marshall Munetsi mwenye umri wa miaka 26 anaweza kutua Brighton kuchukua nafasi ya Yves Bissouma, kiungo wa kati wa Mali aliyehama klabu hiyo na kuelekea Tottenham Hotspur. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# BAYERN YAZIDI KUKOMAA KUMBAKISHA LEWANDOWSKI

●●● Ingawa mshambuliaji huyo ameweka wazi alitamani kuona anatua Barca...

**MUNICH, Ujerumani**

MKURUGENZI wa Michezo wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic amezima mapendekezo ya Robert Lewandowski kuondoka katika klabu hiyo baada ya kumsajili, Sadio Mane.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland ameingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga na ameweka wazi anataka kuhama, huku Barcelona ikiwa ndio klabu anayopendelea kwenda.

Chelsea na Paris Saint-Germain pia zimehusishwa na kutaka kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 33, lakini licha ya nia yoyote ambayo Lewandowski anaweza kuwa nayo kwa mradi mpya, msimamo wa Bayern unaonekana wazi.

Alipoulizwa na Sport Bild kuhusu mapendekezo, Barcelona wanatayarisha ofa ya kumnunua fowadi huyo, alijibu: "Sijali hilo. Natarajia kumwona Robert katika mazoezi pale Sabener Strasse Julai 12."

Salihamidzic kisha aliulizwa kama mustakabali wa Lewandowski sasa umefikia mwisho baada ya kusajiliwa kwa Mane, alijibu: "Ninaelewa swali lako, lakini msimamo wetu uko wazi, Robert ana mkataba hadi msimu wa joto wa 2023."

Mkuu huyo wa Bayern aliweka wazi usajili huo haukuwa wa kugharamia kumpoteza Lewandowski.

Alieleza: "Tulimsajili Sadio ili kuongeza ushindani katika timu yetu.

"Hatukufurahishwa na kutolewa kwetu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya na Villarreal. Tunataka kuimarisha mapambano ya kupata nafasi katika timu yetu.

"Kusajiliwa kwa Mane kutapanga upya nafasi kwa kila mchezaji anayeshambulia. Hatujawahi kufikiria kumwachia mchezaji tulipomsajili Sadio."

BREAKING NEWS
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,008,5

MECHI KALI
SHELBOURNE
VERSUS
DUNDALK FC
1 | 2.89
X | 2.99
2 | 2.39

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# KLOPP AMPONGEZA MANE KWA KUONDOKA LIVERPOOL

**LIVERPOOL, England**

KOCHA Jurgen Klopp amempongeza Sadio Mane kama mmoja wa wachezaji bora kabisa wa Liverpool baada ya uthibitisho wa kuondoka kwake na kujiunga na Bayern Munich.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal alidokeza nia yake ya kuondoka Liverpool baada ya kushindwa kwa klabu hiyo katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid na uhamisho wake wa euro milioni 41 kwenda kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ilithibitishwa Jumatano.

Liverpool tayari wameshapiga hatua katika soko la usajili kujiandaa na kuondoka kwa Mane, kwa kumsajili Darwin Nunez kutoka Benfica, lakini Klopp alikiri ulikuwa wakati muhimu kwa klabu katika kumwenzi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

"Ni wakati muhimu. Hakuna maana kwa mtu yeyote kujaribu kujifanya vinginevyo," alisema Klopp akiiambia tovuti ya klabu.

"Mmoja wa wachezaji bora kabisa wa Liverpool anaondoka na lazima tukubali hili.

"Anaondoka na shukrani zetu na upendo wetu. Anaondoka na hadhi yake kati ya magwiji waliohakikishiwa. Na, ndio, anaondoka katika wakati ambapo yeye ni mmoja wa wachezaji bora katika soka la dunia.

"Lakini hatupaswi kuzingatia kile tunachopoteza sasa, badala yake tusherehekee kile tulichobahatika kuwa nacho.

"Mabao aliyofunga, mataji aliyoshinda; gwiji, bila shaka, lakini pia nyota wa kisasa wa Liverpool."

Mane alishinda kila alichoweza kwa miaka sita aliyokaa pale Merseyside, ikijumuisha taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19 na Ligi Kuu England mwaka 2019-20, akiunda safu ya ushambuliaji ya kutisha pamoja na Roberto Firmino na Mohamed Salah.

Wakati kikosi kizima kilikuwa muhimu kwa ushindi huo, Klopp alimsifu Mane kwa kusaidia kufanikisha yote hayo baada ya kujikita katika maisha ya Anfield haraka baada ya kuwasili kutoka Southampton.

# Vinicius Jr atabiriwa makubwa

**LONDON, England**

VINICIUS Junior atakuwa mmoja wanaongoza katika mbio za kuwania tuzo ya Ballon d'Or mwaka 2023, kwa mujibu wa Rivaldo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, Vinicius alikuwa sehemu muhimu ya kikosi cha Real Madrid kilichoshinda taji la Ligi Kuu Hispania, LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2021-22, akifunga bao pekee katika mchezo wa fainali wakati Los Blancos wakiichapa Liverpool.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 alifunga mabao 22 na kutoa asisti 16 - zaidi ya alivyoweza katika misimu mitatu iliyopita zikijumlishwa - katika michezo 52 kwenye mashindano yote.

Ni Kylian Mbappe (60), Karim Benzema (59), Christopher Nkunku (51) na Mohamed Salah (46) pekee waliohusika katika mabao mengi katika mashindano yote miongoni mwa wachezaji katika ligi tano bora za Ulaya.

Benzema ndiye anayependekezwa zaidi kutwaa Ballon d'Or ya 2022, ambayo itatolewa Oktoba, lakini mshambuliaji wa zamani wa Brazil aliyeshinda Kombe la Dunia, Rivaldo anaamini mwaka ujao unaweza kuwa wakati wa Vinicius.

"Baada ya msimu mzuri akiwa na Real Madrid, ambapo alifunga bao lililoshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, ninatumaini mshambuliaji huyo mchanga wa Brazil ataendelea kuimarika," alisema Rivaldo aakiiambia Betfair.

"Ameimarika sana mbele ya goli na akiendelea hivi anaweza kujidai kuwa nyota wa Real Madrid, kwa sababu Karim Benzema atastaafu siku moja.

"Ni vigumu kutaja wachezaji wanaopewa nafasi kubwa kwenye Ballon d'Or wakati msimu haujaanza, lakini namuona Vinicius hatakosekana pamoja na Kylian Mbappe, Kevin De Bruyne na wengine.

"Mataji ambayo kila klabu itashinda yatakuwa muhimu sana katika chaguo la mwisho."

## HABARI MICHEZO

534,842/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/06/22 | 22:10 | Club Atletico Alvarado vs Belgrano | 3.50 | 2.90 | 2.33 |
| 02. 25/06/22 | 22:30 | Atletico PR vs Bragantino SP | 2.44 | 3.03 | 3.08 |
| 03. 26/06/22 | 00:00 | DC United vs Nashville | 2.43 | 3.40 | 2.85 |
| 04. 26/06/22 | 00:00 | Colon Santa Fe vs Huracan | 2.35 | 3.28 | 3.13 |
| 05. 26/06/22 | 02:30 | Toronto vs Atlanta United | 2.96 | 3.51 | 2.32 |
| 06. 26/06/22 | 05:00 | San Jose Earthquake vs Los Angeles Galaxy | 2.61 | 3.56 | 2.56 |
| 07. 26/06/22 | 05:30 | Portland Timbers vs Colorado Rapids | 2.26 | 3.43 | 3.12 |
| 08. 26/06/22 | 12:00 | Vissel Kobe vs Urawa Red Diamonds | 2.78 | 3.23 | 2.63 |
| 09. 26/06/22 | 12:00 | Nagoya Grampus vs Kashima Antlers | 2.92 | 3.28 | 2.48 |
| 10. 26/06/22 | 12:00 | Yokohama vs Niigata Albirex | 2.59 | 3.24 | 2.74 |
| 11. 26/06/22 | 12:30 | Kyoto Sanga vs Shonan Bellmare | 2.73 | 3.29 | 2.63 |
| 12. 26/06/22 | 13:00 | Omiya Ardija vs Zwiegen Kanazawa | 2.91 | 3.21 | 2.48 |
| 13. 26/06/22 | 19:00 | Ham-Kam vs Sarpsborg | 2.74 | 3.43 | 2.45 |
| 14. 26/06/22 | 19:00 | Sandefjord vs Tromso | 2.78 | 3.42 | 2.42 |
| 15. 26/06/22 | 19:00 | Stromsgodset vs Lillestrom | 2.73 | 3.42 | 2.46 |
| 16. 26/06/22 | 19:00 | San Lorenzo vs Tigre | 2.84 | 3.30 | 2.54 |
| 17. 26/06/22 | 22:00 | Botafogo RJ vs Fluminense | 2.52 | 3.12 | 2.87 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 24/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:30 | 1204 | Melbourne Knights vs ST Albans Saints | 1.52 | 4.11 | 5.08 |
| 12:30 | 2532 | South Melbourne vs Green Gully | 2.03 | 3.43 | 3.18 |
| 12:30 | 5956 | Guangzhou RF vs Changchun Yatai | 13.78 | 5.32 | 1.19 |
| 13:00 | 1896 | Fasil Kenema vs Hawassa Kenema SC | 1.72 | 3.45 | 4.80 |
| 13:00 | 2697 | Daejeon Korail vs Gangneung City | 1.93 | 3.05 | 3.94 |
| 13:00 | 2966 | Kingborough Lions vs South Hobart | 3.48 | 4.12 | 1.75 |
| 13:30 | 5977 | Bentleigh Greens vs Hume City | 1.69 | 3.74 | 4.13 |
| 13:45 | 4253 | West Torrens vs Campbelltown City | 4.03 | 3.93 | 1.67 |
| 14:30 | 4745 | Dalian Aerbing vs Henan Jianye | 8.62 | 4.51 | 1.31 |
| 14:45 | 2897 | Lion City Sailors vs Albirex Niigata (SIN) | 2.25 | 3.68 | 2.60 |
| 15:00 | 2663 | FK Ekranas vs FK Banga B | 1.54 | 3.91 | 5.08 |
| 15:15 | 2987 | Johor Darul Takzim vs Selangor FC | 1.27 | 5.30 | 8.24 |
| 16:00 | 2015 | Vmfd Zalgiris-3 vs Be1 Nfa | 2.25 | 3.29 | 2.85 |
| 16:00 | 2956 | CA Lanus vs CA River Plate (Arg) | 2.31 | 3.15 | 3.00 |
| 16:00 | 4150 | Mekelakeya vs Adama City FC | 2.45 | 2.65 | 3.19 |
| 17:00 | 3292 | Zhenis Nur-Sultan vs FC Zhetysu | 5.70 | 4.13 | 1.47 |
| 17:00 | 3976 | FK Babrungas Plunge vs FK Minija | 1.88 | 3.28 | 3.81 |
| 18:00 | 1514 | Sahab Club vs AL Aqaba | 3.30 | 2.95 | 2.28 |
| 18:00 | 5521 | Germany W vs Switzerland W | 1.22 | 5.35 | 10.89 |
| 18:30 | 4881 | France U19 vs Italy U19 | 2.02 | 3.43 | 3.19 |
| 18:30 | 5331 | Romania U19 vs Slovakia U19 | 2.54 | 3.27 | 2.49 |
| 19:00 | 1267 | Josko Ried vs Olympiakos | 3.65 | 3.65 | 1.89 |
| 19:00 | 4139 | Sturm Graz vs NK Mura | 1.50 | 3.88 | 5.69 |
| 19:00 | 4435 | FC Neptunas Klaipeda vs Riteriai B | 1.22 | 5.70 | 9.63 |
| 19:30 | 1933 | Bruck/Leitha vs SV Lafnitz | 8.05 | 6.48 | 1.22 |
| 19:30 | 2962 | Viktoria Griesheim vs SV Darmstadt | 29.47 | 14.73 | 1.01 |
| 20:00 | 3214 | AB Argir vs Tofta Itrottarfelag B68 | 2.23 | 3.87 | 2.55 |
| 20:00 | 3921 | Denmark W vs Brazil W | 3.00 | 3.35 | 2.14 |
| 20:00 | 4975 | Sola vs Sandnes Ulf 2 | 2.42 | 4.12 | 2.25 |
| 20:00 | 5894 | Dila Gori vs FC Gagra | 1.61 | 3.37 | 5.47 |
| 20:30 | 1390 | Ramtha Club vs Shabab Al Ordun | 2.01 | 3.14 | 3.53 |
| 20:30 | 4357 | EB/Streymur vs Skala IF | 1.82 | 3.59 | 3.69 |
| 21:15 | 2650 | Ukraine W vs Scotland W | 7.07 | 4.91 | 1.32 |
| 21:45 | 1584 | Cork City vs Cobh Ramblers | 1.12 | 7.06 | 15.69 |
| 21:45 | 2066 | Shamrock Rovers vs Bohemians FC | 1.54 | 3.92 | 5.10 |
| 21:45 | 3156 | Waterford Utd vs Bray Wanderers | 1.39 | 4.41 | 6.47 |
| 21:45 | 4563 | Wexford Youths vs Longford Town | 2.56 | 3.39 | 2.42 |
| 21:45 | 4614 | Galway United vs Treaty United | 1.29 | 4.89 | 8.22 |
| 21:45 | 4945 | Drogheda Utd vs Sligo Rovers | 3.25 | 3.20 | 2.09 |
| 21:45 | 5160 | Shelbourne vs Dundalk FC | 2.89 | 2.99 | 2.39 |
| 21:45 | 5914 | UCD Dublin vs Derry City | 9.22 | 5.49 | 1.24 |
| 22:00 | 1715 | B36 Torshavn II vs KI Klaksvik II | 4.02 | 4.70 | 1.57 |
| 22:00 | 4002 | Real Santa Cruz vs Universitario Sucre | 1.82 | 3.63 | 3.63 |
| 22:00 | 4350 | Finn Harps vs St Patricks | 3.08 | 3.18 | 2.17 |
| 22:00 | 5380 | England W vs Netherlands W | 2.30 | 3.24 | 2.80 |
| 22:15 | 2227 | UMF Selfoss vs Fjolnir | 2.74 | 3.63 | 2.18 |
| 22:15 | 3797 | HB Torshavn II vs Undrid FF | 2.51 | 3.69 | 2.32 |
| 22:15 | 4842 | Afturelding vs Thor Akureyri | 2.33 | 3.59 | 2.55 |
| 22:30 | 4222 | Inter Club De Escaldes vs Vikingur Reykjavik | 12.01 | 7.01 | 1.17 |
| 23:30 | 5772 | UTC Cajamarca vs Carlos Mannucci | 1.69 | 3.63 | 4.32 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KMKM, KIPANGA ZAAMSHWA KUELEKEA MICHUANO YA CAF

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar imewataka mabingwa wa Ligi Kuu visiwani hapo, KMKM pamoja na vinara wa Kombe la FA, Kipanga kufanya maandalizi mazuri ili kwenda kufanya vyema kwenye michuano ya kimataifa.

KMKM itashiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Kipanga yenyewe itachuana kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Hayo yalisemwa na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman katika hotuba yake ya kuahirisha Baraza la Wawakilishi Chukwani wakati alipozialika timu hizo pamoja na viongozi wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF).

Suleiman alisema timu hizo zimetwaa ubingwa huo baada ya kuhimili ushindani uliokuwapo msimu mzima, hivyo wanastahili pongezi kwa sababu walipambana na kufanikiwa kutwaa ubingwa huo.

Aidha, ameipongeza ZFF pamoja na Bodi ya Ligi Zanzibar kwa kuendesha ligi hiyo kwa weledi bila ya kuwapo kwa migogoro.

Alisema ZFF imefanya kazi kubwa katika kusimamia uendeshaji wa ligi zake na pia kumaliza ligi bila ya kuwapo kwa migogoro kama ilivyozoeleka.

"Niwapongeze ZFF kwa kuendesha ligi vizuri, ligi imechezwa pasipokuwa na migogoro mpaka imemalizika na kuwapata mabingwa wetu wa FA na Ligi Kuu," alisema kiongozi huyo.

Aliongeza serikali itaendelea kushirikiana na Wizara ya Michezo pamoja na ZFF ili kuhakikisha inaboresha mpira wa miguu visiwani hapo kwa kurejea katika hadhi yake.

Pia amewataka mawaziri na wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kushirikiana kwa pamoja ikiwamo kuwapa ushauri ZFF katika ufanyaji kazi zao, ili kujenga ufanisi zaidi katika kufikia mafanikio.



Mshambuliaji wa Azam FC, Ismail Kader (katikati), akipambana kuwania mpira dhidi ya wachezaji wa Prisons katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam juzi usiku. Azam ilishinda bao 1-0. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Mbeya Kwanza yageukia 'play off'

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchabangwa mabao 4-1 dhidi ya KMC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi, Mbeya Kwanza imesema kwa sasa itajitahidi kushinda mechi zake mbili zilizobaki ili kupata nafasi ya kucheza mechi za mchujo 'play off'.

Kocha Msaidizi wa Mbeya Kwanza, Renatus Shija, alisema baada ya kufanya makosa mengi na kusababisha kupoteza mechi hiyo dhidi ya KMC, matatu yakiwa ya kujifunga, kwa sasa anategemea mechi zilizosalia, huku akiombea Biashara United na Prisons kufanya vibaya ili timu yake ipate nafasi ya kucheza mechi za mchujo na hatimaye kujinasua kwenye janga la kushuka daraja.

"Kwanza kabisa haya magoli waliofunga karibuni yote tumewapa wenyewe na moja la penalti, kwa sababu ya makosa yetu ndiyo yaliyowapa ushindi. Sawa tunakubali tumefungwa, lakini tumebakisha mechi mbili, katika mechi lolote linaweza kutokea, sisi tukashinda mechi hizo na Biashara United na Prisons zikafungwa tukapata nafasi hata ya kwenda kucheza 'play off' ambayo inaweza kutupa mwanya wa kubaki Ligi Kuu kama tukishinda," alisema Shija.

Katika mechi hiyo, wachezaji wa Mbeya Kwanza, Geofrey Muha, alijifunga mara mbili, Rolland Msonjo akijifunga moja, na lingine ni la mkwaju wa penalti uliopigwa na Matheo Anthony.

Goli la kufutia machozi la Mbeya Kwanza lilifungwa na Habib Kyombo ambaye ni kama anaaga, kwa sababu tayari ameshatangazwa kujiunga na Singida Big Stars.

# Michezo

Ijumaa Juni 24, 2022

Nipashe






Bayern yazidi kukomaa kumbakisha Lewandowski

# Jeuri yaendelea kutawala Yanga

●●●Huku taa ya kijani ikimwakia winga Chiko Ushindi baada ya...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nesredine Nabi, akimkingia kifua winga wake, Chiko Ushindi kupewa mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia timu hiyo katika msimu ujao, amesema wachezaji wake wanazidi kuimarika kuelekea mchezo wa fainali ya michuano ya Kombe la FA utakaochezwa Julai 2, mwaka huu jijini Arusha.

Chiko aliyesaini mkataba wa miezi sita na mwisho wa msimu huu unafikia tamati kuhusiana na hatima yake, amekuwa kwenye sintofahamu kwa sababu hajafanya vyema kwa kipindi hicho cha mkataba wake.

Hata hivyo nyota huyo juzi alionyesha kiwango kizuri katika mchezo dhidi ya Polisi Tanzania, ambapo alifunga bao la pili dakika ya 17 huku lile na awali likipachikwa na Feisal Salum 'Fei Toto' kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam kwa mabingwa wapya kuibuka na ushindi wa magoli 2-0.

Baada ya Chiko kufunga bao la pili, Nabi alinyanyuka na kushangilia kwa furaha na kugeukia jukwaa walilokaa viongozi wa Yanga na kuonyesha ishara ya ujumbe kwa viongozi hao kumwandalia mkataba mpya wingа huyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema anataka kumpa nafasi zaidi ya kucheza katika michezo miwili iliyosalia ya Ligi Kuu pamoja na mmoja wa fainali ya Kombe la FA ambapo watakutana na Coastal Union ya jijini Tanga.

Nabi alisema ana matarajio makubwa na Ushindi kwa sababu anajua uwezo wake na ana imani viongozi wa klabu hiyo watafuata mapendekezo yake ya usajili na wachezaji ambao wanatakiwa kubaki.

"Sijaanza kumjua Ushindi hapa Yanga, namjua muda mrefu lakini kuna maisha aliyapitia TP Mazembe ambayo yanatupa shida kuona kile alichonacho, unapomwona mazoezini ni tofauti na kwenye mechi," alisema Nabi.

Aliongeza winga huyo anajua vyema kusakata kandanda ila kutokana na mazingira ya Ligi Kuu Tanzania ilimfanya kushindwa kuonyesha kiwango kizuri na sasa anapambana kuhakikisha katika michezo iliyosalia anamalizia.

Pia alimtaja Ibrahim Baka anatakiwa kuongezewa vitu kidogo ili kumjenga



Winga wa Yanga, Chiko Ushindi (kulia), akiwania mpira dhidi ya beki wa Polisi Tanzania, Datius Peter katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

vyema kwa sababu itasaidia kupunguza gharama za kufanya usajili wa beki mpya kutoka nje ya nchi ambaye anaweza pia akashindwa kuonyesha kiwango kizuri.

Kuhusiana na mechi dhidi ya Polisi Tanzania, kocha huyo alisema haikuwa rahisi sana na hasa kipindi cha pili wapinzani wao waliingia kivingine na kusababisha kushindwa kutengeneza nafasi ya kupata mabao mengine.

"Niwapongeze wachezaji wangu wamepambana na kutumia nafasi vizuri kipindi cha kwanza na kufanikiwa kupata ushindi wa mabao 2-0, kipindi cha pili tulijaribu kufika lakini wapinzani walikuwa makini," alisema Nabi.

Aliongeza alifanya mabadiliko makubwa ya kikosi kwa kuwapa nafasi baadhi ya wachezaji ambao hawajacheza muda mrefu kama ilivyo kwa Baka kucheza na wengine kuwapumzisha.

"Kuumia kwa Zawadi Mauya kumesababisha baadhi ya wachezaji wasipumzike ikiwamo Khalid Aucho na Salum Abubakar (Sure Boy) kutopumzika katika mchezo wa leo (juzi)," alisema Nabi.

Wakati huo huo, kikosi hicho cha mabingwa kiliwasili salama jijini Mbeya kwa ajili ya mchezo dhidi ya Mbeya City utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Sokoine.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli alisema wameamua kuondoka mapema ili kupata muda mzuri wa maandalizi ya kulipokea kombe lao.

"Michezo iliyobaki ni mechi za mazoezi ya kujiandaa na fainali ya Kombe la FA tutakaocheza Arusha, mikakati yetu ni kuchukua makombe yote msimu huu," Bumbuli.

## Simba SC hadi kieleweke Ghana

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

HUKU vigogo wa Simba wakitajwa wako Ghana kukamilisha mchakato wa usajili wa mshambuliaji Augustine Okrah, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Wekundu wa Msimbazi, Barbara Gonzalez amefunguka kuwa, Bernard Morrison hakuwa katika mipango yao kuelekea msimu ujao.

Morrison yuko nchini kwao Ghana kwa mapumziko maalumu, mkataba wake na Simba utamalizika ifikapo Agosti 14, mwaka huu.

Barbara alisema kilichomwondoa nyota huyo ndani ya kikosi cha Simba ni matatizo yake ya utovu wa nidhamu kujirudia rudia.

"Tulimpa Morrison barua ili apate nafasi ya kutafuta timu, hakuwa kwenye mipango yetu tena kutokana na ripoti zake kujirudia rudia hasa zile za nje ya uwanja ... hata yeye anajua Simba hakuna nafasi ya kuongeza mkataba tena," alisema Barbara.

Kuhusiana na mchakato wa ujio wa kocha mpya, kiongozi huyo aliweka wazi tayari wameshafikia makubaliano na mwalimu mpya na watamtangaza wakati wowote hivi karibuni.

"Tumeshapata kocha na tutamtangaza hivi karibuni, kuna maeneo ameshauri tuongeze kwenye usajili, mpaka sasa asilimia 50 za usajili tumekamilisha na tutasajili wachezaji zaidi ya watano," alisema Barbara.

Pia alisema Simba haikuwahi kuwa na mpango wa kumsajili nyota wa zamani wa Asec Mimosas, Stephane Aziz Ki ingawa wanakiri ni mmoja wa wachezaji wazuri kwa sasa.

Ofisa Habari wa Yanga Hassan Bumbuli amesema Simba walikuwa na mpango na mchezaji huyo, lakini wameshindwa.

"Ni kocha wetu aliyeondoka (Pablo Franco), ndiye alimtaja kuwa ni mchezaji mzuri na hii ni kwenye suala ya mpira ni kawaida. Sisi tukimhitaji mchezaji tutasema tu wala hatufichi, mbona Adebayor (Victorien) tulisema? Unajua hii tasnia ya mpira ina propaganda nyingi, asilimia ya vitu wanavyovizungumza vinakuwa si vya kweli, tumetengenezewa barua feki kuonyesha tunamhitaji mchezaji hiyo, we angalia hata leo hii nimekuwa nikipigiwa simu kuambiwa CEO imekuwaje mbona unaondoka? Wakati hakuna kitu kama hicho," Barbara alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >